

# AGANO LA IBRAHIMU

## LIKITHIBITISHWA



Asante, Ndugu Sullivan. Mnaweza kuketi.

<sup>2</sup> Vema kuwa katika nyumba ya Bwana tena, usiku wa leo, mahali hapa panapotumikia kusudi hilo. Nami ninashukuru sana kwa ajili ya nafasi hii ya kuhudumu tena, usiku wa leo.

<sup>3</sup> Jana usiku tulikuwa na wakati mzuri sana, wa kipekee, nilikuwa nao kwa vyovyote vile. Bwana alimimina baraka Zake juu yangu, hata si—sikuweza kulala nusu usiku. Ndipo basi Yeye, nilikuwa nikisoma makala ndogo, mtu fulani aliniandikia barua, na kutuma kipande kidogo kwenye gazeti, naye Bwana akanipa wazo zu—zuri sana juu yake. Kama Yeye akipenda, kesho alasiri nataka kulielezea, papa hapa kwenye. . . kuihubiri kesho alasiri, kwenye mkutano wangu wa alasiri.

<sup>4</sup> Sasa, tuna ninii, sababu ya sisi kufanya, kuwa na *mkutano* wa alasiri. . . Sasa, Ndugu Sullivan alinialika huku kwenye ushirika pamoja na watu wake, na nyinyi watu hapa, naye akaufungua katika ghala ya silaha, ili kwamba kwa jumla usiwe kanisani mwake; nafikiri huo ni uungwana kabisa. Hivi hamwoni hivyo? La kindugu kwelikweli.

<sup>5</sup> Jambo lingine tuliloamua, kwamba tulifikiri lingekuwa ni jambo jema kama hatungekuwa na ibada ya Jumapili usiku, kusudi ninyi watu msikose ibada zenu zozote za kawaida. Mngeweza kuwa na shule ya Jumapili, halafu pia mwe na ibada ya Jumapili usiku. Na baadhi yenu washiriki wa makanisa, la—laiti mngemwelezea mchungaji wenu hilo, kama hayuko mkutanoni, ya kwamba hiyo ndiyo sababu tunafanya hivyo. Hatuko hapa kujaribu ku—kuzuia hu—huduma ya Kristo, tuko hapa kujaribu kusaidia huduma ya Kristo, tukijaribu kufanya yote tuwezayo kushirikiana pamoja katika kila hatua tuwezayo kuwasaidia watu.

<sup>6</sup> Na badala ya Ndugu Sullivan kusema tu, “Vema sasa, tutaufanyia tu kanisani mwangu,” mbona, aliuweka kwenye jumba la mikutano, na ili kwamba kila mtu aweze kuona ya kwamba haikuwa ni nia ya kichoyo.

<sup>7</sup> Halafu basi, badala ya kuufanya Jumapili usiku, tutaufanya Jumapili alasiri, ambao daima ni umati mdogo Jumapili alasiri, kuliko ilivyo Jumapili usiku. Lakini ha—hatuko hapa kwa ajili ya pesa, hatuko hapa kuona ni watu wangapi tunaoweza kuwavutia, tuko hapa tu kujaribu kuweka sehemu yetu kwa ajili

ya Ufalme wa Mungu, kumsaidia kila mtu, hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa hapa.

<sup>8</sup> Sasa, hili haliko kwenye kumbukumbu, wala Ndugu Sullivan hajui kwamba ninajua hili, lakini najua, kufikia wakati huu, amepungukiwa na fedha za mkutano. Sasa, kesho alasiri haitakuwa ni sadaka ya upendo, itakuwa ni sadaka ya gharama. Na kama gharama hazitalipiwa kesho alasiri, nitatuma habari nyumbani, mara moja, kanisani, nasi tutalipia kila senti yake kabla hatujaondoka kwenye jiji hili. Hakutakuwako na chochote kitakachosalia, hakuna madeni tutakayoacha nyuma. Tusipotimiza, tusipolipia gharama kesho alasiri katika sadaka ya upendo... Ifanyi sadaka ya upendo kwa Bwana Yesu badala ya mimi, ili iweze kwenda kulipa madeni.

<sup>9</sup> Sasa, Ndugu Sullivan alikuwa anataka kulipa hayo mwenyewe, bali hatafanya hivyo. La, sitamruhusu afanye hivyo. La, tuta—tutafanya hivyo sisi wenyewe. Na basi kama hakuna za kutosha kumalizia m—mkutano, basi nitaona, nasi tutatuma pesa huku juu kutoka kwa kanisa letu wenyewe huko Jeffersonville kumalizia deni, kumaliza ninii... ili kila kitu kilipiwe, viti, ukumbi, na tangazo, chochote kilichokuwa ndani yake, tutakilipia chote, kuhakikisha kwamba kimelipwa. Haitakuwa za—za—zaidi ya kuwa sawa kwa Ndugu Sullivan, na hao watu.

<sup>10</sup> Sasa, kama mngeweza, laiti mngeweza, kama mchungaji wenu hayupo hapa, kama mngelialika kanisa litoke lije kesho alasiri, utakuwa ni ujumbe wa kinabii ambao ninafikiri kwamba, inaonekana kwangu kwamba Roho Mtakatifu aliweka moyoni mwangu, baada ya kusoma makala moja leo, kwamba ninapaswa kuleta ujumbe huo, kesho.

<sup>11</sup> Na sasa, ndipo ibada zingine nilizo nazo, ni juavyo mimi, ni Jumapili ya Pasaka maskanini, ambako kutakuwa na ibada za ubatizo, na kadhalika. Kisha twende Bloomington, Illinois. Ndugu Sullivan alinialika nikae siku kadhaa za juma lijalo, kama ningeweza, nimechoka sana hata siwezi kufanya hivyo marafiki. Koo langu limekwisha, ni—nimeninii tu, nimekuwa kwenye ibada tangu Krismasi, mnaona, nami nimechoka sana, sana, nami natazamia siku hizi tatu, ama nne, ama tano, zozote zile, ku—kupumzika.

<sup>12</sup> Nami siwezi kukaa nyumbani kufanya hivyo, itanibidi tu kutoka niende mahali fulani na kupumzika, kwa sababu nina Jumapili hadi Jumapili; kisha nitoke huko kwenda Chicago, Jumapili hadi Jumapili; na kisha kutoka huko hadi—hadi Grande Prairie, British Colo- . . . , ama, Alberta; na kutoka huko kwenda—kwenda Dawson Creek, British Colombia; na labda, Fort St. John, kuendelea na kuendelea; na huko chini Miami, Florida; na labda kwenda huko Washington, DC, msimu huu wa kiangazi katika hema kubwa, Bwana akipenda.

<sup>13</sup> Wafanyabiashara kule walituma habari, hivi majuzi usiku, nzuri sana, tulipokuwa Richmond Wafanyabiashara wa Washington, DC walinitumia barua maalum ya kwamba mkutano tuliokuwa nao kule usiku huo, usiku mmoja, ninaamini ulikuwa katika Ukumbi wa Bunge, ama—ama ukumbi fulani huko Washington, wanataka, warudi tena na kupiga hema kubwa mno, nao walisema kama hatukulipia gharama huko Richmond, mbona, kamwe wasingesema lolote kulihusu, wangeilipia wenyewe, Wafanyabiashara Wakristo.

<sup>14</sup> Sasa, hiyo ni kuwaunga mkono kabisa, lakini Bwana akaingia, nasi tukazilipia gharama, kila kitu, yote yalienda sawa huko Richmond, kwa hiyo huenda nikaenda huko juu, kama si mkutano, kwa ajili tu ya ushirika wa hao ndugu wa thamani, ambao mnasimama nao katika—katika nyakati kama hizo.

<sup>15</sup> Sasa, lakini hakikisheni mnakumbuka kesho alasiri, kama...hiyo itaanza, nadhani Ndugu Sullivan tayari ametwambia, saa nane. Na kusema, jambo lingine, kama ha—hatuninii...Ninaamini walisambaza kadi usiku uliopita, ninaamini Billy aliniambia walisambaza kadi jana usiku, namba A, nami nikachelewa sana kuita—kuwaita hapa juu kuwaombea, Nitajaribu kuzifikia usiku wa leo, nikiweza, nisipozifikia, hakika nitazifikia kesho.

<sup>16</sup> Nami nitamwacha aje kesho, halafu alasiri, tunaweza kuendelea kukimbia, tena, tena, tena, baadaye kidogo ikitubidi kufanya hivyo. Tuseme tutaingia saa kumi, vema, tunaweza kuendelea hadi saa kumi na moja, nasi tunaweza kumwombea kila mtu. Halafu basi kama wataninii...Kama mna wagonjwa wowote sasa, ambao mnataka niwaombee, nina hisia ya ajabu sana kuhusu mambo fulani, kwa hiyo afadhali muwalete hapa kesho. Mnaona? Na kwa hiyo huenda ikawa baada ya kitambo kidogo, kwamba hamtanisikia tena, kwa hiyo kama mkitaka niwaombee wapendwa wenu, basi wa—waleteni kesho alasiri, mnaona. Ndipo—ndipo basi tutawapa kadi ya maombi.

<sup>17</sup> Kama wakianza saa nane afadhali mwe hapa yapata saa saba na robo, ama saa saba u nusu, angalau, mnaona. Nami nitamwomba Ndugu Leo, Gene, na Billy, na hao wengine washuke waje na kuwasambazia watu kadi zao za maombi, chochote ninyi...mtu yeyote anayetaka kadi ya maombi. Nanyi mnajua utaratibu, jinsi tunavyofanya, sisi, kesho, labda tutazisambaza tu, kwa sababu tutajaribu tu kuona ni watu wangapi wagonjwa wanaotaka kuombewa.

<sup>18</sup> Sasa, kabla hatujaendelea mbele zaidi, hebu na tuzungumze na Bwana wetu mkuu, wa kifalme, Bwana Yesu, ambaye tuna tumaini letu lisilo na kikomo Kwake na neema Yake ya ajabu. Ni wangapi wangetaka kukumbukwa katika maombi? Fanya tu ijulikane kwa mkono ulioinuliwa. Bwana awabariki, watu wangu, tunapoinamisha vichwa vyetu.

19 Mungu na Baba yetu aliye Mtakatifu Sana na Mwenye Haki, tunakuja Mbele Zako, usiku wa leo, kwa mioyo minyenyekevu na—na roho zilizoandaliwa na tayari kuupokea Ujumbe Wako. Tungekuomba Wewe ututie mafuta, Bwana, kumalizia mlango huu juu ya Ibrahimu, na watoto wake baada yake. Ninaomba ya kwamba utaubariki huu ujumbe usiku wa leo, na mjumbe, na wale wanaoupokea. Jipatie Mwenyewe utukufu, na kama ni mapenzi Yako kwamba tuwaombee wagonjwa, jalia kuwe na wingi wa furaha na nguvu miongoni mwetu, usiku wa leo. Waokoe wale ambao hawajaokoka, waponye wale ambao hawajapona, wajaze na Roho Mtakatifu wale wanaotafuta nguvu na baraka Zako, tupe neema sisi sote. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

20 Ninaamini hao wavulana wamekuwa wakisambaza kitabu kidogo hapa, nafikiri kinaitwa, loo, naam, *Sauti* ya Wafanyabiashara Wakristo. Ni wangapi walio nacho? Hilo ni zuri. Kama huna, kichukue usiku wa leo unapoondoka.

21 Gene, sijui kama ningeweza kukuuliza, ama mtu fulani, wawekeni vijana milangoni, popote wanapotokea, ama mtu fulani. Wanaviuzaje? Vinagharimu senti kumi?

22 Kama huna hizo senti kumi, kichukue kwa vyovyote vile, nitakilipia, mnaona. Ninawatakeni msome ushuhuda huu hapa, wa lile ono. Ninii tu, ninataka kila mtu humu ndani achukue kimoja. Kama ninyi—kama hamwezi, mbona mnidai tu mimi. Na kila mtu ahakikishe amepata kimoja, usiku wa leo. Wao ni—wao ni *Sauti* ya Wafanyabiashara Wakristo.

23 Nao waliandika ono mle ndani ambalo Bwana alinipa hivi majuzi, nalo likauwasha tu moyo wangu. Mimi. . . Hawana yote humu ndani. Ndugu Tommy Hicks, ama, Tommy, siwezi kukumbuka jina lake, mhariri, sasa hivi, Nickel (Asante, Ndugu Gene.), Ndugu Tommy Nickel aliliandika, bali ha—hakuliweka lote mle, bali lilikuwa. . . Hakuweka mle ndani kuhusu wakati nilipomwona nani wangu, sidhani aliliweka mle ndani, kwa vyovyote vile, kuhusu kumwona mbwa wangu, na farasi wangu wakinijia, mnaona. Nafikiri, labda hilo linahojiwa miongoni mwa watu wanapowazia juu ya wanyama kuwa katika Ufalme, bali wako.

24 Wako wapi wale farasi waliokuja, wakamchukua Eliya? Yuko wapi yule ambaye Yesu anakuja, amepanda juu yake, majeshi ya Mbinguni? Mnaona? Ni lini mbwa mwitu na mwana-kondoo watakula pamoja? Mnaona? Hakika. Wanafikiri tu. . . Tunapata tu mawazo yetu mafupi, na—na kama kitu fulani hakiendani na hayo, vema basi, kamwe hatutaki uhusiano wowote nacho; hiyo ndiyo shida. Lakini, hata hivyo, hilo ni sawa. Na kuna ya kutosha mle. . . Halafu mnaona huko chini, ilikuwa na. . . Je, mlisoma maskini, maskini kile kipachikwa hapo chini, kuhusu kufufua wafu?

<sup>25</sup> Sasa kumbukeni, kabla hujachapisha chochote, huna budi kuweza kukithibitisha hicho. Kwa hiyo tuna taarifa zilizoandikwa kutoka kwa madaktari, mameya wa jiji, na kadhalika namna hiyo, ambapo madaktari waliwatangaza wamekufa, na wameondoka kwa yapata muda wa saa nane na saa kumi, kisha wakawa hai tena, kupitia maombi; kwa hiyo ni taarifa iliyoandikwa. Kitabu hiki kinaenda kote ulimwenguni, na kutafsiriwa katika lugha mbalimbali, na kadhalika, kama tu *Reader's Digest*, miongoni mwa Wakristo, na haina budi kuwa ni ya kweli, nawe huna budi kuthibitisha mambo hayo unapoyasema. Inakubidi kuwa. . .

<sup>26</sup> Kwa hiyo yule waliyepata kuthibitisha alikuwa, kabla hajaweza kuandika hayo, alikuwa huko chini Meksiko, yapata miaka mitatu iliyopita nilipokuwa kule chini, na maskini yule mwanamke wa Kihispania, akiwa amebeba yule mtoto mchanga aliyekufa asubuhi hiyo saa tatu, naye Bwana akamfufua saa nne usiku huo mkutanoni, naye alikuwa akirusha mateke chini ya blanketi hiyo. Wakisimama pale, karibu watu elfu thelathini wamesimama tu, wakiegemeana tangu mapema asubuhi hiyo, siku nzima kwenye hiyo mvua, na kadhalika, ili tu kuisikia Injili. Kwa hiyo, watu kama hao ni. . . Mungu atawafanyia watu mambo mengi mno watakapokusanyika namna hiyo, nao wataamini, na kuinyenyekeza mioyo yao mbele za Mungu.

<sup>27</sup> Sasa ninataka kusoma Andiko hilo tena nililosoma jana usiku, maana ninataka kumalizia juu ya somo lilo hilo; wala hatutakaa muda mrefu usiku wa leo.

<sup>28</sup> Sasa, ninyi wageni, hapa, hivi mnajua Maskani ya Full Gospel ilipo, ambapo Ndugu Sullivan ndiye mchungaji? Vema. Hapo ni mahali pazuri pa kwenda asubuhi. Ukiishi karibu na lolote la makanisa haya mengine ya Full Gospel hapa, hapo ni mahali pazuri pa kwenda kusikia Neno la Bwana. Kwa hiyo sasa, hudhurieni shule ya Jumapili mahali fulani, kesho. Shikilieni tu rangi zenu, na mkae kwenye wajibu wenu.

<sup>29</sup> Sasa ninaamini ninasoma kutoka Mwanzo, mlango wa 22, na kifungu cha 14:

*Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-yire: kama watu wasemavyo hata leo, Katika mlima wa BWANA itapatikana.*

<sup>30</sup> Sababu ya mimi kusoma hayo Maandiko ni kwa sababu, kama kile ninachosema hakifanyi kazi, hakika Yale aliyosema Yeye, yatafanya kazi. Neno langu ni neno la mwanadamu, litashindwa; Neno la Mungu ni Neno Lake Mwenyewe, wala haliwezi kushindwa.

<sup>31</sup> Nalo neno *Yehova-yire* linamaanisha, “Bwana amejipatia Mwenyewe dhabihu.”

<sup>32</sup> Sasa, jana usiku, mlifurahia somo hilo juu yake jana usiku? Mwanangu, Billy, ambaye yuko nyuma ya hili jengo

sasa, yeye hurudi kule nyuma kusikiliza aone kama anaweza kusikia, alisema yamegugumizwa sana, sana, mwajua, hu—huwezi kusikia vizuri. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu, badala ya kuhubiri, nilifikiri tu kidogo ningezungumza juu ya Neno kwa muda kidogo, na labda mngeweza kusikia vizuri zaidi kidogo.

<sup>33</sup> Mnaona, maghala haya ya silaha kama hili, majengo tambarare, hayakujengwa kwa ajili ya mikutano kama hii, ni kwa ajili ya mpira wa vikapu, na mazoezi, dari haijatengenezwa vizuri, mfumo wa sauti ni mbaya sana, sana. Lakini tunalishukuru Jesu la Marekani kwa majaliwa ya kuwa na kinga juu yetu usiku wa leo, na kuja mahali hapa, nasi tunawashukuru sana, Bwana na awabariki daima.

<sup>34</sup> Sasa, tulimchukua Ibrahimu jana usiku, na Uzao wa Ibrahimu baada yake. Na, loo, ni baraka ya jinsi gani tuliyo nayo ya kuonyesha! Na, kwangu mimi, mtu yeyote angeweza kuwa na nafsi moja ya shaka kwa njia yoyote, unapooni yale Mungu aliyohidi, halafu yale Mungu aliyofanya? Ni kama tu kusoma Biblia, ambapo inatabiri jambo fulani litatukia, kisha uchukue historia uone mahali lilipotukia.

<sup>35</sup> Sasa, Mungu alisema ya kwamba angebariki baraka hii na ahadi juu ya Ibrahimu na Uzao wake baada yake. Nasi tunaona, hasa kabisa, kila hatua ambapo Mungu alimtembelea Ibrahimu, Yeye alifanya jambo lile lile kwa Uzao wa Ibrahimu baada yake.

<sup>36</sup> Basi tulijikuta wapi jana usiku, ndugu? Tulijikuta mwishoni kabisa mwa barabara, moja kwa moja chini kwenye jambo la mwisho, nalo Kanisa likipokea ishara Yake ya mwisho, na kisha kubariki yote, Yeye akaingia miongoni mwetu, jana usiku, kisha akapitia kote katika kusanyiko na kufanya jambo lile lile alilofanya huko Sodoma. Ni wapi panaweza kuwa na kuteleza? Tunaweza kuwa tumekosea wapi?

<sup>37</sup> Ndipo usiku uliotangulia huo, tuliwapeleka Israeli nyikani, na kuonyesha kile hasa kanisa, Israeli. . . Sasa, tunaona katika Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 10, ilisema ya kwamba mambo hayo yote yaliwapata Israeli kama mifano kwetu. Sasa, tunaona ya kwamba walikuwa ni mifano, kuonyesha yale Mungu aliyowafanyia ni kivuli tu cha. . . yale anayofanya pale, yale aliyofanya, ya kawaida, Yeye anafanya ya kiroho.

<sup>38</sup> Mnaona katika Biblia, mlango wa 12, yule mwanamke katika mlango wa 12 wa Ufunuo, huku mwezi ukiwa chini ya miguu yake, na jua kichwani mwake, ikionyesha sheria ikifikia. Mara jua linapochomoza, mwezi unashuka; mwezi ni mke wa jua. Loo, na—napenda usomaji wa Biblia wa namna hiyo!

<sup>39</sup> Mnaona, jua na mwezi ni mfano wa Kristo na Kanisa. Jua linapotua, halionekani, halijatua, halionekani tu kwa ulimwengu, linaakisi nuru yake mwezini upate kuangaza wakati halipo. Kwa hiyo hivyo ndivyo Kristo alivyofanya alipoingia Utukufuni, Yeye huakisi Nuru Yake juu ya Kanisa Lake, lipate

kutoa Nuru hata atakaporudi. Nzuri sana! Loo, jamani, kuwazia ya kwamba jua, ukitaka, likiakisi nuru yake mwe—mwezini kuonyesha nuru! Nayo nuru. . .

<sup>40</sup> Pia, mwezi wenyewe ni mlinzi, Mungu aliweka mipaka ya bahari, na kuweka mwezi kuiangalia. Nayo bahari, jinsi inavyoruka ukingoni kwa hasira, ingependa kuangamiza kila kitu duniani kwa sababu iliangamiza wakati mmoja, mwajua.

<sup>41</sup> Na kuona dhambi, ikilundikana, hayo ni mawimbi, ikiyagongesha hayo mawimbi makubwa ukingoni. Basi kumbukeni, katika siku za mwisho kulitabiriwa mawimbi ya bahari, bahari ikivuma, mioyo ya watu ikivunjika, hofu, fadhaa ya mataifa, dhiki; hizo zingekuwa ndizo ishara za wakati wa mwisho, tumepitia hayo yote, chini kote barabarani. Sasa sisi hapa, moja kwa moja mpaka kwenye ile ishara ya mwisho kwa watoto wa Ibrahimu, na hata kuyaleta majina ya wale wajumbe, kama tu ilivyokuwa katika wakati wa Ibrahimu, kuonyesha hakuna kuteleza popote, Biblia, BWANA ASEMA HIVI.

<sup>42</sup> Halafu kanisa linaketi limekufa, michezo ya mpira, vivutio vya mji, na mambo ya kilimwengu yamelivutia kanisa kabisa. Biblia ilisema watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wenye mfano wa utauwa. Vyumba vya hoteli vimejaa walevi, hata huwezi kulala, walimu wa shule ya Jumapili, watu wakienda kanisani, washiriki wa kanisa, wakiwa na “burudani safi ya Kimarekani.” Wenye dhambi! Loo, ulimwengu huu wa kale unayumbayumba kama mlevi anayekuja nyumbani asubuhi.

<sup>43</sup> Nini kilitukia? Wakati dhambi hizi zote zinapoanza kuwa kama zile katika siku za Sodoma, wanawake, nusu uchi, wakikimbia kupitia vyumba vya hoteli, na wanaume, wamelewa, wakiwafuata nyuma (Hilo haliko mbali mahali pengine, hilo liko hapa.), halafu basi ni jambo gani linalotukia? Mungu alisema, “Nimeshuka kuja kuona kama taarifa hizi zote ni za kweli.”

<sup>44</sup> Watoto wa kweli wakipaza sauti, “Njoo, Bwana Yesu!” Labda mmoja kwenye mji. Kama tulivyouliza hivi majuzi usiku kama Roho Mtakatifu alivyotuaambia katika Biblia, “Watie muhuri wale tu wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yaliyofanywa mjini.” Wangetiwa muhuri wapi? Kuko wapi kutiwa muhuri kwa watu? Hebu tusidanganyike, hebu tuwe sawa.

<sup>45</sup> Kama yule mzee mweusi alivyosema, wakati mmoja, “Nilimwambia Bwana nataka kulizungumzia pamoja Naye sasa, maana sikutaka shida yoyote mtoni.” Hiyo ni kweli, marafiki, sitaki shida yoyote mtoni. Hujui ni saa ngapi utashuka kwenye mto huo, huenda ukawa huko katika dakika zingine kumi na tano, huenda ukawa huko kabla ya mapambazuko, bali kuna

jambo moja la hakika, unaufikia, kwa hiyo afadhali uwe na hakika sasa.

<sup>46</sup> Mungu hafanyi mambo haya kwa mchezo tu, kwa maonyesho ya jukwaani, Yeye hufanya hivi kwa ajili ya utukufu Wake na heshima Yake, kwa sababu Yeye aliahidi angefanya hivyo. Hebu tusiliangalie kwa urahisi, bali kwa uchaji, kwa busara, na kwa kiasi. Njoo kwenye Chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ungama dhambi zako na kutokuamini kwako, mwombe Mungu akurehemu, kama mwenye dhambi, na kukuokoa kwa ajili ya Kristo.

<sup>47</sup> Wakati mwingine watu huingia kanisani, na kusema, “Si lazima niulize hilo. Mimi tayari...” Loo, yachunguze maisha yako, ewe rafiki, uone jinsi imani yako inavyorekodiwa na Neno. Kumbukeni, hao Mafarisayo hawakufikiri wanahitaji kuokoka, walikuwa ni watu watakatifu, waliojiweka wakfu, walikuwa wahudumu, baba zao walikuwa wahudumu, babu zao, baba wa babu zao, baba wa babu wa babu zao, wote walikuwa wahudumu, waliishi maisha mazuri sana hata alama moja dhidi yao, wangeweza kupigwa mawe kwa ajili yake. Ati kuyajua Maandiko? Waliyajua kikamilifu, naye Yesu akasema, “Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi.”

<sup>48</sup> Mwangalieni Mungu, Yeye alikuwa akiwaonyesha ishara ya Masihi, wala hawakuamini, walisema, “Yeye ni Beelzebuli, mpiga ramli.” Huku wakiwa werevu, na wenye elimu, na kuishi maisha yaliyowekwa wakfu, na hata hivyo walikuwa wenye dhambi. Kwa nini? Hawakufanya uzinzi, hawakuvuta sigara, hawakulewa, hawakuenda kwenye madansi, hawakucheza karata, bali walikosa kuamini, hiyo ndiyo sababu walikuwa wenye dhambi.

<sup>49</sup> Hiyo ndiyo sababu ninaivurumishia Pentekoste siku hizi. Haidhuru unacheza kiasi gani katika Roho na kunena kwa lugha, ninaamini jambo hilo, bali mngeweza kunena kwa lugha kama kumwaga njegere kwenye ngozi kavu ya ng’ombe, na bado mmepotea. Sawa. Hata hamkupata ninii... Nimewaona wachawi wakinena kwa lugha na kucheza katika roho, wakanywa damu kutoka kwenye fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kumwita ibilisi, wakicheza katika roho, na kunena kwa lugha, na kupaza sauti kwa nguvu walivyoweza, bila shaka, huwezi kutegemea hayo.

<sup>50</sup> Kama ungali huamini Neno la Mungu jinsi tu lilivyoandikwa, wewe ni asiyeamini, mwenye dhambi. Mungu hushuka na kutekeleza Neno Lake, na kulidhihirisha, na kulionyesha herufi kwa herufi, ambapo hakuna mtu anayeweza kulipinga, Mungu Mwenyewe hulitetea, ndipo wanaondoka kwa sababu ya kanuni fulani ya imani, si ajabu tumeangamia. Lakini unaweza kulikomesha? Mtu fulani aliniambia, hivi majuzi, “Hivi unaweza kulikomesha?”

Nikasema, “La, bwana.”

Akasema, “Vema, mbona unaninii . . . ? Mbona usinyamaze?”

<sup>51</sup> Nikasema, “Ninaweza je kunyamaza? Naja kwenye Hukumu, sauti yangu itakuwa kwenye santuri kule ambayo itakwaruza hiki kizazi chote.” Siwezi kunyamaza. Ole wangu kama nikinyamaza! Nina . . .

Nikasema, “Huamini katika kutenda dhambi, sivyo?”

Akasema, “La.”

<sup>52</sup> Nikasema, “Vema, kwa—kwa nini unahubiri dhidi yake? Kwa nini wewe . . . ? Kama—kama unajua ulimwengu utaendelea katika machafuko hayo, kwa nini uendelee kuhubiri?” Hatuna budi kutoa sauti dhidi yake, hatuna budi kufanya hivyo; ukweli hauna budi kujulikana.

<sup>53</sup> Mungu ni mwenye haki, Yeye hutoa onyo Lake. Kwa nini Nuhu alisimama mlangoni akihubiri wakati Yeye alijua hawakuwa wakiingia? Aliandaa safina kwa ajili ya wokovu wa nyumba yake, hivyo ndivyo ilivyokuwa, lakini ilimbidi kutoa Ujumbe vivyo hivyo. Mungu ni mwenye haki, Mungu alijua hawatakuja, Yeye alijua kabisa watu wanane wangeokolewa katika siku za Nuhu, kama tu vile katika ule wa mwisho, kama vile Yeye ajavyo kizazi hiki. Anajua ni nani atakuja na ni nani hatakuja, lakini Yeye—Yeye anajua ilivyokuwa, hiyo ndiyo sababu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Mnaona?

<sup>54</sup> Nasi tunajua tunaishi katika wakati wa ajabu sana, lakini we—wewe unawajibi— . . . Moyo wa—wako unalia tu, huwezi kutulia, huna budi kulisema.

<sup>55</sup> Sasa, angalieni yale aliyomfanyia Ibrahimu, akiuonyesha Uzao wake, ndipo mtaelewa ya kwamba mambo haya hayapaswi kupelekwa kwenye vifundo vikuu vya mishipa. Wa—watu hapa . . . Karibu watu wote ninaokutana nao, wanatazamia uamsho mkubwa mno, mpana, utakaoenea ulimwenguni, hayo yamepita, tuko mwisho.

<sup>56</sup> Wanatarajia miujiza mikubwa na ishara kwa sababu tu hawaijui Biblia. Hao ni wale manabii wawili wa Ufunuo 11, watalisimamisha jua, Elisha na, ama, Musa na Eliya, hiyo ni baada ya Kanisa la Mataifa kuondoka. Hiyo ni kweli. Mnaona, hiyo ni katika Wayahudi, wakati Mungu atakapowageukia Israeli tena. Wakati huu wa kanisa, soma Ufunuo 1 hadi 3 ndipo utalipata, utaona kile anachoupa huu wakati wa kanisa, kule kuitwa watoke, ishara ya mwisho ilikuwa ni kuonekana kwa Eliya tena jukwaani, hatimaye, wakati wa mwisho. Nasi tu—tuko, tunajua kwamba, ya kwamba kila kitu alichosema kitakuwa jinsi tu Yeye alivyosema.

<sup>57</sup> Sasa, tunaona ya kwamba ambapo Yeye alimwita katika ninii ya 3 . . . katika mlango wa 12 wa Mwanzo, na kumhesabia

haki kwa imani, kwa sababu Ibrahimu alimwamini Mungu. Hiyo ni kweli?

<sup>58</sup> Sasa, sisemi hili...Sasa, siwataki mnukuu hili tena miongoni mwa watu wenu, lakini mnaona, kila kitu katika Biblia kinasafiri katika tatu, *tatu*, kikikifanya *kimoja*. Sasa, kama vile ka—katika Biblia, imeandikwa humu ndani ya kwamba...Mnajua Mungu aliandika Biblia tatu. Mnaamini hilo? Aliandika moja angani, moja katika piramidi, hiyo nyingine kwenye karatasi. Sasa, tunajua ya kwamba wanatengeneza ubao wa uaguzi kutokana na piramidi; wanaunda ubao wa uaguzi kwa Zodiaka; wanatengeneza ubao wa uaguzi kutoka kwenye Biblia, bali hiyo haizuii kweli Zake, kweli Zake ni sawa kabisa.

<sup>59</sup> Sasa, kama ukiangalia katika Zodiaka, umbo la kwanza katika Zodiaka ni lipi? Ni bikira. Umbo la mwisho katika Zodiaka ni lipi? Leo yule simba. Kule kuja mara ya kwanza, na kuja mara ya pili kwa Kristo, Yeye alikuja kwanza kwa bikira, anakuja tena Simba wa kabila la Yuda, kisha samaki waliopindana, wakati wa kansa tuliomo sasa, kabla tu ya wakati huo kutukia.

<sup>60</sup> Tunaangalia ile piramidi, ilijengwa *hivi*. Lakini mnaona, lile jiwe la kuwekwa juu kamwe halikuwekwa kwenye ile piramidi. Uliwahi kuwazia hilo? Una noti ya dola mfukoni mwako? Angalia inavyosema, “Ule Muhuri Mkuu,” ile piramidi, na hebu angalia juu yake, lile jiwe, lile jiwe la kuwekwa juu kamwe halikupatikana. Kwa nini? Lile Jiwe la kuwekwa juu lilikataliwa, Kristo.

<sup>61</sup> Angalia hapa chini katika wakati wa Luther, kuhesabiwa haki, nafasi kubwa humu ndani. Kumkiri tu Kristo kulimaanisha kukatwa kichwa chako. Walipotoka kwenye upagani, kichwa chako...ungekatwa kichwa kwa ajili ya ushuhuda wenyewe wa kusema ulikuwa Mkristo, Luther. Basi ilifanyaje? Inalundikana sasa, kwa walio wachache, inashuka karibu zaidi. Nini kilifuata? Utakaso, ndipo ukaitwa mlokole, mtakatifu anayejibingirisha, ama kitu fulani, huo ni wakati wa Wesley. Ni nini kilifuatia? Ndipo ukaja Upentekoste, ubatizo wa Roho Mtakatifu, ninii, Kanisa bado likawa dogo zaidi katika uchache. Na sasa, linaendelea mpaka hilo halina budi kufikia mahali pakamilifu sana, mpaka hatimaye wakati litakapokuja lile Jiwe la kuweka juu, litatoshea kikamilifu kabisa, Kanisa litakuwa, halina budi kuwa katika u—umbo mkamilifu sana, mpaka wakati Kristo atakapokuja Yeye ataingia moja kwa moja ndani Yake. Kweli.

<sup>62</sup> Kwa hiyo mnaona, kunena tu kwa lugha, na kucheza katika Roho, hiyo ni huko chini kabisa mstarini hapa bado. Lile Kani-...Basi kumbukeni, kama uliwahi kuwa kule, huko Misri, kwenye sfiniksi ama piramidi, hayo mawe, huko mbali hewani,

yakiwa na uzito wa mamia ya tani, nayo yamewekwa pamoja kikamilifu, mpaka wembe hata hautaninii... yamechongwa kikamilifu, mpaka yanaumana kikamilifu bila saruji.

<sup>63</sup> Hivyo ndivyo Kanisa litakavyopaswa kuwa, limechongwa sana, Neno likilichonga Kanisa, mpaka Kristo atakapokuja kulichukua Kanisa, ile huduma, Kanisa litaimarika moja kwa moja, nalo litawafufua Luther, Wesley, Pentekoste na wote, na kunyakuliwa pamoja Naye, hiyo ni kweli, kulitwaa Kanisa.

<sup>64</sup> Sasa, wakati, tunaona katika kuhesabiwa haki kile Yeye alichofanya kilikuwa, kwa ule Uzao, ama, kwa Ibrahimu, kilianza na Luther, utakaso, mlango wa 15, wakati alipothibitisha lile agano kwa damu, mlango wa 17 alimtoa Roho Mtakatifu, ule wakati wa Kipentekoste, kwa sababu, mnaona, vitu hivyo vingine vyote vilikuwa kitu kilicho nje ya yale Kanisa lilichopokea kutoka Kwake, kile Ibrahimu alichopokea kutoka Kwake. Lakini aliposema, “Mimi ni El Shaddai,” lile ziwa, akimkaribisha Ibrahimu aje anyonye nguvu zake kutoka kwenye titi la Mungu, auvute Uzima wa Mungu ndani yake, hapo ndipo Kanisa lilipompokea Roho Mtakatifu, wakati lilipoonja U—Uzima wa Mungu, wakati lilipoingiza ndani Yake ubatizo wa Roho Mtakatifu.

<sup>65</sup> Basi Yeye alifanya nini? Kimaandiko tu, kama tulivyolithibitisha jana usiku, tukichukua kile kile... Hebu lifuatilieni, Mungu hawezi kukiuka sheria Zake Mwenyewe. Hiyo ndiyo sababu alimchukua Mwanawe Mwenyewe, katika mlango wa 17 wa Mathayo, na kumpandisha juu ya Mlima wa Kugeuka Sura, na kumweka mahali Pake, kama sheria Yake ilivyokuwa; alifanya hivyo. Halafu basi, alipofanya hivyo, ndipo tunaona, Yeye alifuata sheria Zake Mwenyewe, na hapa akamchukua Ibrahimu vivyo hivyo. Ndipo mnasema, “Una hakika na hilo, Ndugu Branham, kifungu cha 4 na cha 5?” Naam, bwana.

<sup>66</sup> Mnaona, alipompa Ibrahimu sehemu ya Jina Lake, akaweka jina lake mahali pake kwenye hundi, kama vile Lake lilivyokuwa... Lake ni *Elohimu*, *Ibrahimu*. Mnaona? Akampa sehemu ya Jina Lake Mwenyewe. Kuna ufunuo mkuu hapo, nanyi mnatambua ningeweza kwenda mbali zaidi ya hapo, lakini Kanisa, wakati linapaswa kuwa likila nyama ngumu, lingali linakunywa maziwa. Sawa. Kwa hiyo, Yeye alimpa Jina Lake Mwenyewe, *Ibrahimu*, na ndipo alipofanya hivyo, jambo lingine alilofanya baada ya kumpa jina hilo, aliweka hilo kwenye jina lake, basi Yeye alifanya nini? Alimpa ishara ya kwamba alikuwa tayari kuharibu kabisa dhambi zote zilizomzunguka, na kuuandaa mwili wake upate kumpokea Mwana aliyeahidiwa ambaye alikuwa amemngojea, yale hasa Yeye amelifanyia Kanisa.

<sup>67</sup> Ishara ya mwisho aliyompa Ibrahimu ilikuwa ni nini?

Alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, na kumwambia Sara yale aliyokuwa akifanya na kuwazia ndani ya hema.

<sup>68</sup> Naye Yesu, yule Mzao wa kweli wa Ibrahimu, yule Nabii halisi, wa kweli, yule Mungu-Nabii, aliyekuja duniani na kudhihirisha ishara ile ile hadi mwisho wa Wayahudi, wazia hilo, wakati alipokuja duniani, alifanya nini? Alimwambia Simoni, “Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona,” mtu ambaye hangeweza kuandika jina lake mwenyewe, naye Simoni akatambua upesi, kwa mafundisho ya baba yake, ya kwamba Masihi anakuwa na ishara kama hiyo, ndipo akamtambua na kumpokea.

<sup>69</sup> Filipino, mara alipoona jambo hilo, alikimbia, akamwambia Nathanaeli, naye Nathanaeli akaja ukingoni pamoja naye, na kukimbia kule alikokuwa Yesu, naye Yesu akamtazama, na kusema, “Wewe ni Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake.”

Akasema, “Ulinijua lini Wewe, Rabi?”

Kasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona.”

Basi yule mwana halisi wa Mungu, aliyeteuliwa, aliyechaguliwa tangu zamani alisema nini? “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.”

Kasema, “Heri wewe.”

<sup>70</sup> Ndipo anashuka kwa mwanamke huko Samaria, kwa sababu Wasamaria walikuwa wakimtazamia, mwajua, walikuwa wakimtazamia Masihi. Mtu yeyote anayemtazamia Masihi, Yeye atakuja, kama uko hapa ukimtazamia usiku wa leo, Yeye atakutana nawe. Lakini kama humtafuti, Yeye ata—Yeye—Yeye ataninii . . . Yeye pia hakutafuti, kama humtazamii, Yeye kamwe hatakuja kwako. Lakini Wasamaria walikuwa wakimtazamia.

<sup>71</sup> Sasa, kuna jamii tatu tu za watu duniani, Watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, Myahudi, Mmataifa, na Msamaria, na uzao wote ulitokana na hao wote.

<sup>72</sup> Na sasa, mwangalie Petro akiwa na zile funguo, kuthibitisha hilo sasa, Petro akiwa na funguo za Ufalme. Ni wangapi wanaamini yeye . . . Mungu alimpa funguo? Yesu alimpa, hakika alimpa. Naye alizitumia lini? Katika Matendo 2, kwa Wayahudi. Kisha akashuka moja kwa moja kwa Wasamaria, ingawa Filipino alikuwa ameshuka na kuwabatiza katika Jina la Yesu Kristo, lakini hawakuwa wamempokea Roho Mtakatifu bado, kwa sababu Petro alikuwa na funguo. Akashuka, akaweka mikono yake juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu.

<sup>73</sup> Halafu basi, baadaye, kizazi kinachofuata ni kipi . . . tabaka linalofuata ni lipi? Mataifa. Naye akapanda juu na kuifungua Injili kwa Mataifa. Na kutoka hapo, hapakuwapo na haja tena

ya funguo za Simoni Petro, maana tayari ilikuwa imefunguliwa kwa ulimwengu wote.

<sup>74</sup> Sasa, Mataifa hawakuwa wakimtazamia Masihi yeyote, bali Wayahudi na Wasamaria walimtazamia. Yeye alijitangazaje Mwenyewe? Jambo lile lile alilofanya huko Sodoma. Aliwafanyia nini Wasamaria? Wakati huyo mwanamke alipotoka, yule mwanamke aliyekuwa na, yule kahaba, alipokuja kisimani, ama, yule mwanamke aliyeishi katika uzinzi, alikuwa na waume sita, watano alikuwa amewaacha huku akiishi na mmoja wakati huo, basi akaja kisimani kuchota maji, ndipo Yesu akamwona, Naye akasema, “Mwanamke, nipe maji ninywe”:

<sup>75</sup> Naye akasema, “Wewe... si desturi, sisi, tuna ubaguzi hapa. Wewe ni Myahudi, nami ni mwanamke Msamaria, hupaswi kuniomba kitu kama hicho. Hatuna uhusiano wowote, sisi kwa sisi.”

Akasema, “Lakini kama ungejua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji nywe.”

Basi mazungumzo yakaendelea mpaka akawasiliana na roho yake, ndipo akasema, akaona alichotaka, Yeye akasema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Mwanamke akasema, “Sina mume yeyote.”

Akasema, “Umesema kweli, kwa kuwa umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

<sup>76</sup> Akasema, “Bwana,” msikilizeni mwanamke huyu, sasa huyu ni Msamaria, kasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Sasa, tunajua ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya.” Hiyo ilikuwa iwe ndiyo ishara ya Masihi.

Naye Yesu akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

<sup>77</sup> Naye alifanya nini? Akaangusha mtungi wa maji, akakimbilia mjini, na kusema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?” Nayo Biblia ilisema watu wa mji huo walimwamini Yesu kuwa ndiye Masihi, kwa sababu alikuwa amemwambia yule mwanamke mambo aliyokuwa amefanya.

<sup>78</sup> Sasa, hebu taja wakati mmoja alipofanya hivyo kwa Mmataifa, kamwe hakufanya hivyo. Lakini Yesu alisema wakati Mataifa, ama... Ma—Ma—Mafarisayo, na wahubiri wa siku hiyo, walisema Yeye alikuwa wa roho mbaya akifanya hivyo, kwamba Injili Yake haikuwa ya kweli, kwa sababu wao... Alikuwa akiyararua makanisa yao na madhehebu yao, akiwaita kizazi cha majoka na kadhalika, mbweha, na kila kitu ambacho angeweza kuwazia, alikuwa akiwapasua kwelikweli.

<sup>79</sup> Lakini hata hivyo, Yeye alisema, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, msiniamini Mimi, bali nikizitenda kazi za Baba Yangu, basi ziaminini hizo kazi.” Hiyo ni kweli kwa mtu yeyote,

Mungu asipoiunga mkono huduma yake, basi si huduma ya Mungu.

<sup>80</sup> Angalieni basi, mwanamke huyu, alisema, “Njoni, mwone Mtu huyu,” nao watu wa Samaria wakaamini hilo, hakufanya hivyo mara moja zaidi, alilifanya wakati mmoja tu, lakini huyo mwanamke alikuwa... aliwaambia hao wanaume kwamba Yesu alifanya hivyo. Kwa njia ya mtu mwingine, kupitia kwa huyo mwanamke, mji mzima ukamwamini Yesu, kwa sababu ya mwujiza huo mmoja.

<sup>81</sup> Sijui itakuwaje kwa Marekani? Huyu kahaba atasimama kwenye Hukumu na kuwahukumu makumi ya mamilioni ya washiriki wa kanisa kwenye Hukumu, maana si mara moja tu, bali limetendeka mara maelfu mara maelfu kote nchini, kote ulimwenguni, imechunguzwa na sayansi, kila mkosoaji ingeweza kupitia imepitia, na bado anatokea safi asilimia mia moja, Roho Mtakatifu, Neno likiiunga mkono. Tutasimama wapi, ndugu, kwenye Siku hiyo? Liwazie tu. Na hiyo huenda ikawa ni kabla ya asubuhi, tuko mwisho; nitafafanua hilo zaidi kesho.

<sup>82</sup> Angalieni, Yeye alimweka, akampa ishara, kile alichokuwa, nanyi mnakumbuka, ilikuwa ni Mungu Mwenyezi, Haikuwa ni huyo *mtu*, huo ulikuwa tu ni mwili wa binadamu pale, uliotoweka katika muda mfupi tu, bali ilikuwa ni Mungu, akijitambulisha Mwenyewe kwa Kanisa Teule, lililoitwa litoke, lililotengwa. Kumbukeni, si mji wa kimadhehebu, sio jiji, bali ni kundi lililokuwa likizungukazunguka jangwani, likishika njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Kama kawaida, imembidi Mungu kuwaita watoto Wake nyikani, na mbali na mambo haya.

<sup>83</sup> Akamwita, akamwonyesha ishara hiyo, na kusonga mbele, naye Ibrahimu akaamini na mara akabadilishwa. Wakati yule Malaika alipoondoka jukwaani, Ibrahimu alikuwa na mwili uliobadilishwa, na kuwekwa tayari, ndipo yule mwana aliyeahidiwa akaja.

<sup>84</sup> Moja ya siku hizi, ile Injili ya mtindo wa kale mnayosikia itanyamazishwa moja ya siku hizi, nalo Kanisa litapokea mwili, uliotukuka. Itakubidi kuwa na mwili wa namna hiyo upate kwenda juu na kumlaki hewani, hatuwezi kwenda katika mwili wa namna *hii*. Kwa hiyo wale wanaotazama, wale wanaosikiliza, wale wanaozingatia ndio watakaobadilishwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, na kunyakuliwa pamoja kumlaki Bwana hewani, Mwana wa Mungu anayetarajiwa, ambaye tumemtazamia tangu tuliponinii... tunaweza kutambua ya kwamba tulikuwa Wakristo.

<sup>85</sup> Kumbukeni, tulithibitisha jambo hilo jana usiku, jinsi alivyoshuka kwenda Gerari, jinsi ambavyo Sara, mwanamke mkongwe mwenye umri wa miaka mia moja... Kwa kawaida, ninapata barua moja ama mbili kutokana na hilo, zikisema,

“Vema, waliishi tu maisha marefu zaidi.” Lakini ninawatakeni mwone mlango wa 18, na mlango wa 17, pia, Biblia ilisema walikuwa na umri mkubwa, wameinama, wamekunjamana, wakongwe. Basi waliposhuka kule chini, Abimeleki, yule mfalme, akimtafuta mchumba huku ana wanawake hao wote warembo wa Kifilisti, na hata hivyo akampenda huyu nyanya wa nyanya wa nyanya mkongwe sana, sana, sana, naye angemchukua kama mke, lakini Mungu akamlinda.

<sup>86</sup> Nataka uone hapa, jambo fulani, dada, unajua Sara alimpenda Ibrahimu sana hata yeye, mwanamke huyo mrembo, hata akamwita bwana wake? Ambalo Paulo baadaye anasema, “Ninyi ni binti zake, mradi mnaitii ile kweli.”

<sup>87</sup> Sara hakuvalia katika mitindo ya siku hizo, kama alivyofanya Bibi Lutu. Yeye labda alikuwa ndiye kiongozi mkuu wa mashirika yote yaliyokuwa kule chini, mumewe alikuwa meya wa jiji hilo. Kwa hiyo, nadhani alikuwa, katika kanisa lao kubwa, asubuhi wakati kengele zilipolia, nao wote wakaenda huko nje, ninawazia alikuwa mwanamke aliyejulikana sana; hakutaka kuacha hayo, alikuwa amefungwa na dunia.

<sup>88</sup> Hivyo ndivyo watu siku hizi, hawataki kusikia kuhusu kuja kwa Bwana Yesu. Mbona, ndilo jambo tukufu sana ninaloweza kuwazia, Kwake kupasua anga sasa hivi! Acheni tumalizane nayo. Kwa nini nisibadilishe uzee huu wa kale uliokauka, wenye makunyanzi, uliipasuka ambao umejaa uharibifu, hakuna kitu ila mabuu ya ngozi yangeweza kuula, na kuichukua nafsi hii hapo ndani inayompenda Mungu, na kuungana katika William Branham mpya kabisa mwenye umri wa miaka ishirini na mmoja ambaye kamwe hatakuwa mzee, na kamwe, kamwe hatashikwa na huzuni, wala hatakufa, hatashikwa na ugonjwa kamwe, kuishi pamoja na Wateule katika nyakati zote katika Milele yote? Loo, nisingeweza kuwazia jambo kubwa zaidi!

<sup>89</sup> Hiyo ndiyo sababu ninawatakeni msome ushahidi huu hapa, kitu hiki kidogo, niliona jambo hilo, ninajua ni kweli, nilipeana mikono kule, na—na, na watu waliokuwa... ambao niliwajua. Nami ni—nilikuwa nimesimama nikijiangalia, nimelala pale kitandani, nami huyu hapa nimesimama, si mbali sana, hatutakuwa na umbali sana wa kwenda, maana nilikuwa nimesimama hapa halisi tu kama ninavyosimama kwenye mimbara hii. Ndipo nikawazia, “Sasa hapa, mimi huyo hapo nimelala *pale*, basi ningewezaje kuwa nimesimama *hapa*?” Kama tu nilivyo sasa hivi. Kulikuwa na watu, kila mmoja wao ni mrembo, ninaweza kuwaona hao wanawake.

<sup>90</sup> Kwa namna fulani nimekuwa mkali kwa wanawake, lakini si—simaanishi ninyi wanawake Wakristo, Ninamaanisha wale wanaotenda kana kwamba wao ni Wakristo wala sio, mnaona, wanaotaka kuwa Mayezebeli, la, bwana, kuyafuata mambo ya ulimwengu. Hakika ninawakemea, nami ni—ninaninii tu, sina

budi kufanya hivyo, siwezi kujizuia. Lakini huna budi kuwa na mbaya kumfanya mzuri kunawiri; huna budi kuwa na usiku kufurahia mwanga wa mchana; huna budi kupata mabaya kuthamini mazuri. Yote yanafanya kazi pamoja kwa manufaa ya Mungu, na utukufu Wake, mko kwenye uwanja wa vita si uwanja wa mandari.

<sup>91</sup> Vita! Kila mtu asema, “Njoo, uwe Mkristo, kila kitu kitaenda sawa.” La, bwana, sivyo kwa Mkristo, “Wote wanaoishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu watateswa.” Huna budi kuchekwa, na kudhihakiwa, kukanyagwa, kupigwa teke, kudhihakiwa, “Kama walimwita Bwana wa nyumba Beelzebuli, ni zaidi sana vipi watawaita wanafunzi Wake?”

<sup>92</sup> “Nitashika njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa, nilianza pamoja na Yesu, Ee Bwana, nipitisha.” Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo ninii yangu—hiyo ndiyo ninii yangu—hiyo ndiyo njia yangu mbadala nitakayopitia.

<sup>93</sup> Kama nikiangalia tu chini usiku wa leo, na kuangalia hapa katika mji huu, niangalie kwa miezi mitatu iliyopita ambapo nimekuwa kote nchini na kuona kule kuanguka kwa makanisa, kutokujali kwa wachungaji, kuona kutokujali miongoni mwa watu wanaotoka, wanaoonekana kama samaki na mikate, na—na kitu kidogo cha kwanza wana hasira ya kutosha kupigana na msumeni unaovuma, na wasiojali, wabaya, Wapentekoste, shirika la wahudumu linataka kuniondoa kwenye ulingo kwa sababu tu nilimruhusu mtu mmoja jukwaani ambaye hakubatizwa jinsi walivyodhani anapaswa kubatizwa, na—nao... Loo, kutokujali kiasi hicho! Kama ningekuwa nikiangalia papa hapa, ni—ningekata tamaa. Nina furaha Mungu alinishika kabla kanisa halijanishika, wakati nikitafuta habari za Mungu. Hiyo ni kweli. Niligundua ya kwamba Mungu alikuwa halisi.

<sup>94</sup> Bw. Baxter, wakati mmoja, Ern Baxter, alikuwa akisimamia mikutano yangu, alisema huko Canada, walikuwa, wakati mmoja kulikuwa na shindano la kushindania baiskeli mpya ya Schwinn. Walikuwa na ubao ambao ulikuwa na upana wa futi moja, iliwabidi kuiendesha kwa umbali wa yadi hamsini, ama mia moja, wakiwa yapata futi tatu hewani. Na kila mmoja wao pale alikuwa bingwa, Ern akasema, “Ningeweza kwenda mjini, ninunue vyakula vya mama yangu, niviweke chini ya mikono yangu, na kupitia karibu na magari ya mtaani, karibu na hayo magari pasipo kuugusa mpini wangu kamwe.” Kasema, “Ningeweza *kuendesha*.” Aketi kinyumenyume juu yake, na kuendesha vile tu angeweza kuendesha mbele, kasema, “Haikuleta tofauti yoyote kwangu.” Na karibu wote walikuwa mabingwa, nao walikuwa na hakika walikuwa wanaenda shinda hiyo baiskeli ya Schwinn.

<sup>95</sup> Nao walikuwa na maskini jamaa mmoja dondoadume

miongoni mwao, hakuwa mwendeshaaji mzuri sana, walijua hatashinda. Lakini walipowaweka wote njiani na kuwaanzisha, kila mmoja wao alianguka, ila maskini mvulana huyu dondoandume, aliendesha mpaka mwisho, akashuka, akapokea lile tuzo, akaichukua hiyo baiskeli. Nao jamaa hao wote wakamzunguka, wakasema, “Tuambie jinsi ulivyofaulu.”

<sup>96</sup> Kasema, “Jamani, nitawaambia mahali mlipokosea.” Kasema, “Niliyawazia yote kabla sijaingia kule.” Hilo ni wazo zuri. Akasema, “Mnaona, ninyi nyote mlikuwa mkijaribu namna *hii* kuweka baiskeli kwenye ubao, mkiangalia baisikeli yenu moja kwa moja chini namna *hii*, ikawatia wasiwasi, mkaanza kuyumbayumba, mkaanguka. Basi nikaona mahali mlipokosea.” Akasema, “Kamwe sikuangalia kilichokuwa *huku* chini, niliangalia tu mwisho na kukaa imara.” Jambo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo! Angalieni mwisho na kujiimarisha, mwendeele tu kusonga mbele.

<sup>97</sup> Ningevunjika moyo usiku wa leo, kama haikuwa kwa jambo hilo, ninaangalia mwisho, kujiweka tu imara. Songa mbele, haidhuru ni jambo gani linalotukia, endelea tu, usiangalie hilo, endelea tu kuangalia mwisho, huko ndiko unakokutana na Mungu kule chini mwishoni, huko ndiko thawabu zinapotolewa. Usiangukie *hapa*, endelea hadi mwisho. “Mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka,” Maandiko.

<sup>98</sup> Sasa, tunaona basi ya kwamba thibitisho la, la Ibrahimu, lilitoa. . . Na kila kitu kilitendeka sawasawa kabisa, sasa. Sasa angalieni, sheria moja ambayo Mungu alilipa Kanisa Lake, hakuna hata moja—hakuna jambo hata moja alilomwahidi Ibrahimu, hakuna hata jambo moja alilomfanyia Ibrahimu, ila ambalo amefanyia, ama, amelipa Kanisa, isipokuwa jambo moja, kubadilishwa mwili. Na atakapofanya hivyo. . .

<sup>99</sup> Sasa kumbukeni, ilibidi Sara abadilishwe. Ni wangapi wanaamini hilo? Inua mkono wako. Ilibidi awe na mwili uliobadilishwa. Alikuwa na umri wa miaka mia moja, angewezaje kuzaa mtoto?

<sup>100</sup> Ibrahimu, vema, Biblia ilisema, kama mwanadamu angeninii, mwili wake ulikuwa umekufa kwa miaka mingi. Soma Warumi mlango wa 4, ambapo ilisema, “Ibrahimu hakuuhesabu mwili wake, uliokuwa umekwisha kufa, wala hali ya kufa ya tumbo lake Sara. Hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu, akimtukuza Mungu,” akaendelea tu kusonga mbele.

<sup>101</sup> Sasa, mwili wake haukuwa na rutuba, tasa, umri wa miaka mia moja, na umekufa, kijinsia. Tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa, lisilozaa, mishipa ya maziwa imekwisha, matiti yamekwisha. Nao moyo, ati mwanamke huyo mwenye umri wa miaka mia moja apate utungu wa kuzaa? Mnaona, kulikuwako. . . Alikuwa tu kama aliyekufa, lakini basi

asingeweza kumpata mtoto huyo, asingeweza kupokea ahadi hiyo, isipokuwa abadilishwe.

<sup>102</sup> “Sasa, unajaribu kusema nini, Ndugu Branham?” Sikilizeni kwa makini, hatuwezi katika miili ya namna hii, kumpokea Mwana aliyeahidiwa, kwa kuwa Yeye haji duniani, tunapaswa kutwaliwa juu. Miili yetu inapaswa kubadilishwa, katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, nasi tutanyakuliwa kumlaki Yeye hewani. Nayo ishara ya mwisho iliyotolewa, kabla ya yale maangamizi, ilikuwa kwamba yule Malaika, akionyesha ya kwamba Mungu angekuwa akiishi katika mwili wa mwanadamu, akifanya ishara ile ile, kabla miili yetu haijabadilishwa, na hiyo ndiyo ishara ya mwisho Kanisa linapata.

<sup>103</sup> Nionyeshe jambo moja zaidi ambalo Mungu alimfanyia Ibrahimu, nionyeshe ishara moja zaidi aliyompa ila ile ishara pale, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho. Wote wanaojua hilo, walio wasomaji wa Biblia, waseme, “Amina.” Hiyo ndiyo ishara ya mwisho iliyotolewa; hii ndiyo ishara ya mwisho. Kanisa, nisikieni, katika Jina la Bwana!

<sup>104</sup> Angalieni elimu yangu, upungufu wangu wa kuhubiri, bila kushikilia somo langu na kuzungumza kama aliyetiwa mafuta, ama, wahubiri wenye elimu kweli wananavyo. Msisikilize hayo, sikilizeni yale ninayowaambia, Neno la Mungu, Mungu yuko nyuma yake, kwa sababu amethibitisha Neno linalohubiriwa. Kama huwezi kuniamini, unasema, “Vema, wewe, Ndugu Branham si wa dhehebu letu,” vema, aminini kazi hizo basi, achaneni na madhehebu, na kuamini hizo kazi. Lipelekeni kwenye dhehebu lenu wenyewe, wafanyeni waliamini, mngeweza kufanya kazi bora zaidi wakati huo, kuliko niwezavyo mimi, ama unaweza kumshinda Mungu kufanya hivyo, Mungu hawezi kuifanya Mwenyewe.

<sup>105</sup> Angalieni, mlango wa 18 ndipo alipofanya jambo hili. Mlango wa 17 sasa, Yeye alimpa nguvu kwa ajili ya huo mwujiza, akampa Roho Mtakatifu, kwa maneno mengine, akamwacha anayone Uzima Wake, wa Mungu Mwenyewe ndani yake.

<sup>106</sup> Sasa, tunafanya nini tunapompokea Roho Mtakatifu? Tunachukua Uzima wa Mungu ndani ya wetu. Hiyo ni kweli? Nini: tunachanganya Uzima wa Mungu katika wetu. Sisi ni wana wa Mungu, kwa sababu tunavuta kutoka kwa Mungu, Roho Mtakatifu ambaye hutufanya wana wa Mungu. Hilo linafanya nini? Linatufanya tayari basi, kwa ajili ya badiliko. Loo, ndugu, linatufanya tayari kwa ajili ya badiliko linalokuja, kujazwa na Roho. Egemea tu moja kwa moja kifuani Mwake, na uendelee kunyonya. Ndipo tutabadilishwa moja ya siku hizi, hiyo ni mara moja, pia, ninaweza kuahidi hilo, Mwana aliyeahidiwa yuko njiani Mwake.

<sup>107</sup> Sasa angalieni, mara baada ya jambo hilo, Sara akapata mimba, naye alijua atampata mtoto huyu. Sasa, yeye ni kijana sasa, mrembo, hata mfalme alimpenda. Ingembidi awe mrembo sana, la sivyo mfalme huyo asingalimpenda kamwe, mwajua, alikuwa mwanamke mrembo, naye alitaka kumwoa, ndi—ndipo Mungu akamlinda.

<sup>108</sup> Jambo moja zaidi ninalotaka kulielezea kanisa, sasa, baadhi yenu mlioketi hapa, jana usiku wakati upako uliponigusa, ningeweza kuhisi hiyo miali midogo mle ndani, nimekuwa nikijaribu kuliwazia, nililiandika hapa chini kusudi nisilisahau, nilishika hilo jana usiku, kwamba mnawazia, “Vema, ni—nilifanya *hivi na vile*, nilifanya *hivi na vile*.” Mara nyingi, ninaona watu hata hawataingia kwenye mstari wa maombi, hata hawatachukua namba yao wanapoitwa, wanahofia hiyo itaitwa, mambo fulani. Sasa, nilikuwa nikikemea hayo moja kwa moja, nyote mnajua hilo, na sivyo isipokuwa kwa kweli niongozwe kufanya hivyo, sifanyi hivyo tena.

<sup>109</sup> Sasa, mtafanya makosa yenu. Unasema, “Ndugu Branham, haidhuru ningefanya nini, kamwe nisingestahili.” Hiyo ni kweli. Lakini angalia, unasema, “Ndugu Branham, wakati mmoja sikuamini Ujumbe huu.” Hiyo ni kweli, na—nakisia wengi wenu hawakuamini, nisingeamini, nadhani, mimi mwenyewe, nisingeweza kuamini isipokuwa Mungu anifunulie Hilo. U—ungekuwa na...Ni ufunuo, Kanisa lote limejengwa juu ya ufunuo, bila ya ufunuo hutauona kamwe, wewe ni kipofu.

<sup>110</sup> Yesu...Biblia ilisema, ninaamini, Mathayo 12, ninaamini ndipo, ambapo alisema, “Ingawa Yesu alikuwa amefanya miujiza mingi mbele yao, hata hivyo wasingeweza kuamini, kwa sababu Isaya alisema, ‘Wana macho, wala hawawezi kuona; masikio, wala hawawezi kusikia,’” na watu watakatifu kwelikweli, walio watakatifu hasa. Kwa hivyo utakatifu sio yote, kuishi kitakatifu sio yote, imani ndiyo kitu muhimu.

<sup>111</sup> Sasa sikilizeni, enyi kanisa, ninataka kuingiza hili humu ndani, maana ninaamini Roho Mtakatifu aliniambia nifanye hivyo, huenda mmekei hapo, ambapo baadhi yenu wameketi, ninajua mnaninii, hamkubaliani nami, sasa hivi, sasa naweza kulitaja jina lako ukitaka nitaje, kwa hiyo, ninajua hilo, lakini pia ninaweza kuona mbali zaidi ya hapo, kwamba utaamini hilo moja ya siku hizi.

<sup>112</sup> Kwa hiyo nitaingiza tu jambo hili, mpate kuelewa, ili niweze kuwapa mahali padogo pa neema hapa, wakati haitachukua muda mrefu sana, mpaka mtakapobadilisha nia yenu, baadhi yenu, baadhi yenu hamtabadilisha. Lakini kumbukeni, Sara alipomsikia Mtu huyo kwa mara ya kwanza, ambapo yeye ni mfano wa Kanisa, aliposikia hayo, alipoona ishara hiyo ikitendeka kwa Ibrahimu, kwa kweli alilicheka hilo moyoni mwake, naye hakuliamini na akalishuku kuwahi kuwa hivyo.

Hiyo ni kweli? Wakati huo, Mungu angelifuta jina lake. Hiyo ni kweli? Lakini Yeye asingeweza, yeye ni sehemu ya Ibrahimu, wao ni mmoja.

<sup>113</sup> Na kama kweli hujachochewa, hujasisimkwa katika mhemuko, huna kanuni fulani za imani za kanisa, bali kweli ulimpokea Roho Mtakatifu, na wewe kweli ni sehemu ya Kristo, na ungali una shaka kidogo niani mwako, Mungu hatakusukumia mbali na hayo, kwa sababu Yeye hawezi, wewe ni sehemu ya Kristo, Yeye atakuleta kwenye ile kweli.

<sup>114</sup> Sasa, kama hujawahi...umeninii tu, huenda ulinena kwa lugha, ukacheza katika Roho, na kufanya mambo haya yote pale, hiyo—hiyo haimaanishi una Roho Mtakatifu. Loo, jamani, jamani, hiyo ni maili milioni moja mbali naye. Yesu kamwe hakusema, “Sasa kumbukeni, ninaamini ya kwamba mnapopokea utimilifu wa Roho Mtakatifu, mnanena kwa lugha.” Sawa. Lakini Yesu kamwe hakufanya hivyo, hakuna Maandiko katika Biblia yanayosema ya kwamba hilo ni thibitisho la Roho Mtakatifu; ninawatakeni mlitoe, kama ndivyo. Hakuna Maandiko kama hayo.

<sup>115</sup> Yesu alisema, “Kwa tunda lao mtawatambua.” Na tunda la Roho si kunena kwa lugha, hiyo ni karama ya Roho Mtakatifu, baada ya Roho Mtakatifu kuja, hiyo ni moja ya karama zinazoambatana Naye. Kuhubiri, kunena kwa lugha, kufasiri lugha, mambo hayo yote ni karama za Roho Mtakatifu.

<sup>116</sup> Walishangaa kwenye Siku ya Pentekoste, Petro alisema, “Tubuni, mkabatizwe, kila mmoja wenu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea Kipawa cha Roho Mtakatifu.” Mnaona?

<sup>117</sup> Sasa, lakini kumbukeni, ninaamini ya kwamba unapojazwa sana na Roho Mtakatifu wewe—wewe...Biblia ilisema, “Midomo ya watu wageni na lugha nyingine nitasema na watu hawa.” Kugugumiza, umejaa Roho Mtakatifu sana huwezi kusema lolote katika lugha yako mwenyewe, hapo ni wakati unapojazwa na Roho Mtakatifu. Lakini ninaamini ya kwamba unapomwamini Mungu kwa moyo wako wote, na kumkubali Yesu kama Mwokozi wako, una sehemu ya huyo Roho Mtakatifu, maana Yesu alisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele.” Na kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele. Ndipo wewe ni mtoto tu, ndipo unaanza kutembea ukaingia katika utimilifu wa Roho. Unakua katika neema, ndipo wewe ni...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

<sup>118</sup> ...Wesley, na sasa katika Pentekoste, jambo lile lile, kisha kuwekwa kwa mwana, halafu ile karama ya mwisho ya ishara, kisha kunyakuliwa kwa mwili, kubadilishwa kwa mwili, na Kunyakuliwa.

<sup>119</sup> Sasa, waliporudi, Sara alitambua alikuwa mja mzito. Loo, hapana shaka alikuwa maskini mama mwenye furaha. Ninaweza kumwona sasa, hizo nywele nyeusi, zinazometameta, hayo macho makubwa, ya mahameli, uso mzuri, alikuwa ni kijana mwanamke wakati huo, labda katika miaka yake ya ishirini ya mwanzoni. Ibrahimu, mwenye nguvu na mwenye afya, kijana mwanamume, aliyebadilishwa kutoka jamaa mzee, aliyevunjika, akawa kijana mwanamume, akionyesha yale atakayoufanyia Uzao wote wa Ibrahimu, hiyo ni kweli kabisa.

<sup>120</sup> Halafu basi, muda si muda mwajua, wangeweza kuwa, kuishi kama vijana. Ndipo wakamzaa mtoto huyu mdogo, na wakati alipokuwa na yapata umri wa miaka kumi na miwili, Mungu akasema, “Sasa, ili kuwahakikishia watu wote jambo hili, nitawathibitishia kile nitakachofanya, kuonyesha ya kwamba Uzao wa Ibrahimu kamwe hautalitilia shaka Neno Langu, Uzao wa kweli wa Ibrahimu hautalitilia shaka Neno Langu.”

<sup>121</sup> Sasa, hii hapa njia ya kupima kama wewe kweli ni Uzao wa Ibrahimu, ama sivyo: Kanisa linaposema, “Amini *hilo*, nami nitakufukuza,” hilo halimaanishi chochote kwa Uzao wa Ibrahimu, hata kidogo, hilo linamweka tu njiani mwake vizuri, hilo linamweka tu huru, huyu hapa anaenda.

<sup>122</sup> Na, kwa kuwa alikuwa—alikuwa awe baba wa mataifa, sasa, Mungu alisema, “Ninataka umchukue huyu mvulana wako, nami nitakuonyesha katika ono unaelekea kwenye *kilima cha namna gani*, mlima, nawe umpandishe mvulana huyo kule juu, na kumwangamiza kabisa.”

<sup>123</sup> Ungeweza kuwazia kile kilichoingia akilini mwa Ibrahimu kama mwanadamu *hapa* juu, *hapa* juu? “Vema, nitakuwaje baba wa mataifa, na hapa nimengojea miaka hii yote na kumpata mvulana huyu hapa, naye huyu hapa mwenye umri wa miaka kumi na miwili, ananitoa nje sasa, na kusema, ‘Mtoe nje ukamwue?’ Vipi...? Naye aliniahidi ya kwamba kupitia kwa mvulana yuyu huyu, huyu ndiye yule mvulana Yeye aliniahidi kupitia kwa Sara, na kama—kama ningalikuwa na mvulana huyu hapa, yeye angekuwa baba wa mataifa, sasa Yeye ananipeleka nje kumwua.”

<sup>124</sup> Hapo ndipo mambo ya kiakili yanapoanza kufanya kazi, lakini maskini huyo nyuki akaendelea kusema, “Uliamini nini miaka ishirini na mitano kwa ajili yake, hata hivyo?” Maskini nyuki huyo alisema, “Vema...”

<sup>125</sup> Ndipo ikatokea kwenye, koo lake, kisha akakiri, “Nilimpokea kama mtu kutoka kwa wafu, nimeshawishika kabisa ya kwamba Mungu anaweza kumfufua kutoka kwa wafu.” Jambo ndilo hilo. Wakati *hili* linapoanza kuzungumza hapa chini, *hii* inanyamaza.

<sup>126</sup> Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, katika bustani ya Edeni ibilisi alichagua sehemu moja ya mwanadamu, naye Mungu akachagua sehemu moja; Mungu aliuchagua moyo wake, ibilisi akachagua akili zake. Na sasa, siku hizi, kanisa siku hizi, linategemeza kila kitu juu ya akili, kamwe haliwazii ya moyoni. Mnaona? Na kitu pekee wanachoweza kuona, “Vema, kamwe siwezi kuliona hivyo.” Huoni kwa macho yako, hata hivyo, unaangalia kwa macho yako, unaona kwa moyo wako. Ukiangalia chochote, useme, “Sikioni kabisa.” U—unakiangalia, bali *hukioni*, inamaanisha *hukielewi*, ufahamu wako unatoka moyoni mwako.

<sup>127</sup> Sasa, huyu hapa sasa, ha—halielewi kwa akili zake, atafanyaje jambo hilo? Akili zake zingemwambia hivyo, hizo ni hoja zake, bali Biblia ilisema, “Tunatupilia chini hoja.” Zitupilie mbali nasi. Wasema, “Nitapataje kupona wakati daktari anasema, ‘Wakati nimefanya *hivi*...?’” Hilo halina uhusiano wowote nalo.

<sup>128</sup> Unapata kama mtu mmoja katika kila mia tano ambaye kweli anaamini hilo, wamekaa moja kwa moja pale, wala hakuna kitu ulimwenguni kitakachowabadilisha. Vema, inatubidi kufanya nini? Kuchambua kila kitu, mpaka tutakapompata huyo. Hiyo ni kweli. Mungu huchunguza kote duniani kumpata mtu mmoja. Ee Mungu! Ninapowazia hilo, linaufanya moyo wangu kuwaka moto. Mungu anaichunguza dunia kujaribu kumpata mtu mmoja atakayejisalimisha Kwake, daima amefanya hivyo.

<sup>129</sup> Alimpata mtu mmoja katika siku za Nuhu, kutoka kwenye makumi ya mamilioni na mamilioni. Watu wanataka, kama tu vile, kuna watu wengi sana kama Samsoni siku hizi, Samsoni alimpa Mungu nguvu zake, bali asingempa moyo wake; Mungu angeweza kutumia nguvu zake, bali si moyo wake. Samsoni alikuwa kwa namna fulani mtu wa wanawake, mwajua, naye asingeweza kumpa Yeye moyo wake, ilimbidi kumpa huo Delila, lakini alimpa Mungu nguvu zake. Mungu alitumia nguvu zake, bali asingeweza kuutumia moyo wake.

<sup>130</sup> Wengi sana siku hizi, Mungu, utampa Mungu akili zako, “Nitakujengea nyumba kubwa, nitakuundia dhehebu, nitafanya *hivi*, nitafanya *vile*.” Hivi hamtambui hilo ndilo jambo lile lile Kaini alilofanya na akakataliwa?

<sup>131</sup> Kaini alijijengea madhabahu, akatoa sadaka, na kusema, “Hii hapa, nitakuabudu, ninakuamini. Hiyo *hapo* sadaka yangu, hiyo hapo *madhabahu* yangu, ichukue ama uiache.” Huyo ndiye huyo mtu siku hizi, mtu wa kidini, Esau vivyo hivyo, na kanisa vivyo hivyo. “Nimefanya *hivi*, nimefanya *hivi*, nimefanya *hivi*.” Si yale umefanya, ni yale Yeye aliyofanya. Mpe moyo wako, na umfuate.

<sup>132</sup> Anajaribu kutafuta mtu atakayemfuata. Alikuwa na mmoja wakati huo, Ibrahimu, alikuwa ni mtu yule mkamilifu, lolote Mungu alilosema, hilo lilikuwa sawa.

<sup>133</sup> Kwa hiyo angalia, ungeweza kuwazia, sasa, Ibrahimu asingeweza kumwambia Sara, mke, maskini mvulana huyo wa Kiyahudi, mwenye sura nzuri, mwenye umri wa kama miaka kumi na miwili, atamchukua, na kukata koo lake? Hilo lingekuwa ni jambo baya sana kumwambia Mama, asingeweza kumwambia. Kwa hiyo, kesho yake asubuhi akaamka, na kukata kuni, akasema alipasua kuni, ambalo linamaanisha “alizikata,” akaziweka kwenye gunia la namna fulani, namna fulani ya gunia la ngozi, akaziweka mgongoni mwa nyumbu, na kuwaita watumishi wawili, na kusema, “Isaka, mimi na wewe tunaenda kuabudu, hebu tuwachukue nyumbu pamoja nasi. Mama, tutarudi baada ya siku chache.” Vema.

<sup>134</sup> Anaenda mbele, huyo anapanda kuelekea milimani. Basi kumbukeni, alienda safari ya siku tatu. Hiyo ni kweli? Siku tatu. Sasa, mtu wa kawaida, mtu yeyote tu. . . naye ni kijana, labda umri wa miaka ishirini, ishirini na mitano. Nilipokuwa nikishika doria, nilitembea maili thelathini na mbili kila siku kupitia misituni, nasi tumezoea kuendesha magari wakati wote. Yote aliyofanya mwanadamu wakati huo kwa ajili ya usafiri, ama ni kupanda nyumbu, au—au—au kutembea. Kwa hiyo, ninaweza kutembea. . . Hatimaye ningeweza kusema, milimani alitembea angalau maili ishirini kwa siku. Vema, baada ya kutembea siku tatu huko nyuma, ndipo akainua macho yake na kuona mlima aliouona katika ono, ukiwa mbali, kisha akaufikia. Angalia mahali alipokuwa sasa, kutoka kwenye ustaarabu. Ninapenda hili, hili ni zuri sana, msilikose.

<sup>135</sup> Walipofika mlimani, Ibrahimu aliwaambia wale—wale wavulana waliokuwa wamewashika nyumbu, akasema, “Nyinyi kaeni hapa, waangalieni nyumbu, mimi na kijana, tunaenda kule kuabudu, na mimi na kijana tutarudi.”

<sup>136</sup> Utasemaje hilo, Ibrahimu, wakati unaenda kule kumwua mvulana huyo? Ni kitu gani? Hiyo ndiyo imani hiyo. Hajui jinsi litakavyotukia, bali anajua litatukia. Loo! Loo! Loo! Loo!

<sup>137</sup> Unasema, “Ndugu Branham, unatenda kijinga huko juu.” Vema, labda ninatenda kijinga, lakini ninajisikia vizuri sana. Ninajisikia vizuri zaidi hivi, kuliko nilivyojiskia katika maskini mambo ya akili za kimwili, kwa hiyo afadhali nibaki hivi.

<sup>138</sup> “Ninyi wavulana ngojeni hapa pamoja na nyumbu, mimi na kijana tunaenda kule kuabudu, kisha tutarudi.”

Vipi kama Malaika angesimama pale, na kusema, “Ibrahimu. . .”?

Loo, vipi kama ibilisi angesimama upande mmoja, kasema, “Ibrahimu, umesema uongo?”

139 “Loo, la. Kuna *kitu hapa* ndani kinachoniambia hata kama itanibidi kumwua, nilimpokea kama mtu kutoka kwa wafu, Mungu angeweza kumfufua kurudi duniani tena. Mimi na huyu kijana tutarudi, kwa sababu gani? Mungu tayari aliniambia ya kwamba kupitia kwa mvulana huyu kungekuwako na Uzao ambaye angeyaokoa mataifa. Ndipo akabadilisha jina langu na kuweka *h-i-m-u* mwishoni mwa jina langu, nami ni baba wa mataifa kupitia kijana huyu, nami sijui lile Mungu atakalofanya kule, bali Yeye atalifanya.”

140 *Whiu!* Loo, jamani, hilo linawasha moto! Hiyo inakupa kitu cha kusimamia. Hiyo si moja ya hadithi hizi za Katoliki, za Baba Krismasi za kitu fulani cha kubuni ambacho hakijawahi kutukia, hiyo ni BWANA MUNGU YEHOVA ASEMA HIVI. Amina. “Haileti tofauti yoyote kwangu jinsi tunavyorudi, tutarudi. Hivyo tu.”

141 “Jinsi wewe...?” Sasa, kama Yeye angesema kuninii... Huyu hapa mtu, ameketi hapa na fimbo, kipofu, “Utapokeaje kuona kwako, bwana?” Acha tu Mungu anene na moyo wake wakati mmoja, kisha uone kitakachotukia. Labda kuna mmoja kule aliye na kansa, anayekufa; mmoja hapa nyuma mwenye ugonjwa wa moyo, ndio kwanza afanyiwe uchunguzi, daktari alisema, “Hawezi kuishi, atakufa,” acha maskini nyuki huyo azunguke hapa chini wakati mmoja, “Mimi ni Bwana nikuponyaye, ayafunguaye macho yako, aondoaye kansa, anayekufanya utembe.” Huh! Yote yamekwisha. Sijali mambo yoyote ya kisayansi, chochote kile, haidhuru kama daktari akiweka ninii, akimfanyia uchunguzi wa moyo, na kumwambia moyo wake ulikuwa tayari umesimama, angali angeamini hilo. Naam, bwana. Yeye atafanya hivyo kwa vyovyote vile, hakuna kitu kinachoweza kulizuia, hiyo ndiyo—hiyo ndiyo imani.

142 Mnajua nini? Samahani, ndugu, dada, Sijui ni kwa nini nitasema jambo hili, lakini lina—linanikaba roho kulisema. Ninajua jambo fulani liko karibu kutukia kwangu, kwa hiyo nina—ninajiondolea tu mzigo. Hiyo ni kweli. Utukufu kwa Mungu! Ndugu, nimeona mambo mengi sana ya imani ya kujifanya, ya ajabu-ajabu, *inayoitwa* imani ya Kimarekani, hata yananichefua tumboni mwangu. Wainjilisti wakiwapitisha watu mistarini, na kusema, “Loo, *ihisi!*” Utafanyaje jambo hilo?

143 Nilipata barua kutoka Ujerumani hivi majuzi, ya mhudumu Mlutheri wa Kijerumani, kiongozi wa shirika huko Ujerumani, katika wilaya fulani ambapo mwinjilisti mmoja alikuwa, naye akavutia usikivu wa mwinjilisti huyu kwake, kasema, “Jambo ulilofanya ni kuwanyang’anya watu pesa. Na ingekuwa bora kama ninyi Wamarekani msingekuwa huku.” Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, ninakubaliana naye. Kasema, “Vipi kuhusu maskini Deborah Stadsklev, huko juu, kama ukisema imani hii yote ya ajabu-ajabu ni ya kila kitu?”

<sup>144</sup> Nina barua mumu humu kwenye faili. Lolote ninalosema kutoka hapa, ndugu, ninaweza kuliunga mkono. Mnaona? Akasema, “Imani hii yote hapa uliyokuwa ukisema kwamba unayo, kwa nini ninyi nyote mlifanya mitetemeko hiyo yote, na kurukaruka, na kadhalika pale, mkijaribu kuwaambia watu wameponywa, nao wakafanya *hivi*, na kufanya *vile*, wakati hawakuponywa? Kamwe hamkuleta toba yoyote.” Kasema, “Kwa nini hukungojea kama Ndugu Branham alivyofanya, walipompigia simu kuhusu maskini Deborah Stadskev? Alingojea mpaka akapata jibu dhahiri kutoka kwa Mungu.” Haya basi.

<sup>145</sup> Ngojeni mpaka mtakaposikia, BWANA ASEMA HIVI. Myasafishe maisha yenu, mwachane na kutokuamini kwenu, mwache kuwa na hii *ajabu-ajabu*, “Nilihisi, ninagusa, nina damu, nina...” Loo! Si ajabu kitu hicho kinazama! Hakina budi kurudi kwenye Biblia ya Mungu, kutubu kutokana na kutokuamini, si mambo ya *ajabu-ajabu*, kupiga makofi, na kuingiza mihemuko mingi. Mahali pa kuzaliwa kwa Wapentekoste ni katika hayo, siku hizi, kuwatikisa, na kusema, “Liseme! Liseme! Liseme! Liseme! Liseme! Liseme!” mpaka wanasema ni namna fulani ya lugha isiyojulikana, ama kupata machafuko, ndipo waseme una Roho Mtakatifu, na kuishi maisha ya namna yoyote, wakiwa na kutokuamini kwa kutosha ndani yao ambako kungeipaka jehanamu yote ya ibilisi. “Imani ya ajabu-ajabu.” Ha!

<sup>146</sup> Nina shida gani, hata hivyo? Ninawaambia tu ukweli, siku moja mtaipata, siku moja mtajua ya kwamba nimewaambia ukweli, sauti yangu huenda ikanyamaza. Hu—hu—huenda mkaweza kuunyamazisha mwili unaonena, bali kamwe hamtainyamazisha sauti hiyo, inatoka kwa Mungu. Walimpiga Stefano mawe, bali wasingeweza kuukomesha Ujumbe wake. Utaendelea, kanda hizo zitachezwa baada ya mimi kuondoka kwa miaka mingi.

<sup>147</sup> Naam, “imani ya ajabu-ajabu,” ya Kimarekani, imejengwa chini ya fadhaa nyingi, wanawake waliojipodoa waliovaa kaptura na kadhalika, wakikimbia mistarini, na kuwatikisa, wakiipiga mayowe, “Naam, umeipata, haleluya, wewe!” Loo, upuuzi. Tubuni! Mrudieni Mungu. Tunahitaji kusafishwa. Amina.

<sup>148</sup> Msifikiri nina hasira, sina hasira. Kama ningekuwa nimekasirika, ningeshuka niende pale madhabahuni, nitubu kabla sijamaliza Ujumbe huu. Ninawaambia tu jambo fulani moyoni mwangu linalochemka, Nalo ni Neno la Mungu. Mnahitaji kusafishwa kutoka mimbarani hadi kwenye orofa ya chini, kote.

<sup>149</sup> “Imani ya ajabu-ajabu,” hakuna kitu kama hicho kwa Mungu. Imani ya Mungu ni safi, dhahiri, isiyoghoshiwa. Hiyo ni

kweli. Kitu fulani ndani, kikitembea, kinasema, “Ninalikubali.” Ndugu, unajua mahali ulipo basi.

<sup>150</sup> Hapa si muda mrefu uliopita, huko chini kabisa Kentucky, Ndugu Sullivan, shati kuukuu, lenye viraka, la samawati, macho ya chuma ya kijivu, aliniangalia kwenye jicho, na kusema, “Mhubiri, ninaamini hilo.” Loo, ndugu, hiyo ilikuwa asilimia mia moja na zaidi; aliamini. Nayo kansa, iliyoning’inia kwenye shavu lake ikaanguka sakafuni, aliamini. Wengi sana wana matumaini badala ya imani. Sasa, magazeti yalichapisha makala yake, mwandishi wa habari amesimama pale, nayo hiyo kansa ikafingirika miguuni mwake, asingeweza kujizuia kuandika habari zake, aliokota mwenyewe.

Kasema, “Mbona usininii . . . ? Sikuiona, popote.”

<sup>151</sup> Yesu alisema, “Angalieni msimwambie mtu.” Tuna matangazo mengi sana siku hizi, kujibunia kitu fulani mbele ya umma kukifanya . . . Loo, afadhali ninyamaze, niendele. Angalieni, lakini hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

<sup>152</sup> Ibrahimu alimchukua maskini jamaa huyo mdogo, angalieni, akaweka kuni juu ya mgongo wa Isaka. Mfano wa Kristo akiwa na ubao mgongoni Mwake. Hao wakapanda mlimani, wakapanda juu, wakafika mpakani mwa misitu, wakapanda juu miongoni mwa miamba mikubwa, huko juu kabisa kwenye majabali makubwa, kwenye mchanga uliopauka, wakapanda juu ya huo mlima, ambapo hakuna kitu ila tu mizabibu ya kale, na vitu vilivyozungushiwa kwenye visiki, ama, miamba. Akajifingirishia mawe kumi na mawili pamoja, akaziweka hizo kuni chini, akachukua moto, akawasha sada- . . . , uh, akawasha madhabahu.

Maskini Isaka akashikwa na shaka, akasema, “Baba yangu?”

Akasema, “Mimi hapa, mwanangu.”

Akasema, “Hii hapa madhabahu, kuni zipo, moto upo, lakini yuko wapi mwana-kondoo, ama sadaka?”

<sup>153</sup> Akasema, “Mwanangu, Mungu atajipatia Mwenyewe mwana-kondoo kwa sadaka hii.” Haya basi. “Jambo pekee ninalofanya ni kufuata tu maagizo, ni juu ya Mungu kumtoa huyo mwana-kondoo.”

<sup>154</sup> “Nitapataje kuona kwangu? Nitawezaje . . . ?” Hilo silo swali, fuata tu maagizo, ukiamini bila kushindwa. Mungu atajipatia Mwenyewe mwana-kondoo kwa ajili ya sadaka.

<sup>155</sup> Kisha akasema, “Isaka, weka mikono yako nyuma yako.” Akachukua kamba na kuanza kuifunga mikono yake, Isaka alijua wakati huo. Angalieni utiifu wake, kama vile Yesu Mwana wa kweli wa Mungu, utiifu hata kufa, alijitwika msalaba. Akamfunga mikono na miguu yake, Ibrahimu akamwinua maskini mvulana huyo na kumlaza juu ya mwamba.

156 Ninaweza kumwazia akisimama pale, na kujaribu, akili zake zikijaribu kuingia kazini, “Utamwambia nini Sara utakapofika nyumbani?”

157 “Mimi—mimi. . .” Lakini maskini yule nyuki akaendelea kusema, “Mimi ni Yehova, nitatoa. Nifuate tu Mimi.” Mnaona, mambo mawili yakifanya kazi, wakati ule ule. Utasikiliza nini? Ukisikiliza *hili*, umekwisha; ukisikiliza *hili*, huwezi kwenda, huna budi kuwa na hakika (Hapa.), ni kamilifu.

158 Sasa, akavuta nywele zake kutoka usoni mwake, akakichukua kichwa chake, akakirudisha nyuma kusudi koo liwe tupu, akafungua maskini shati lake na kulivuta nyuma, kusudi koo lake lipate. . . kasema, “Laza kichwa chako nyuma kidogo, Mpenzi, kwa ajili ya Baba.”

159 Unafikiri hilo lilikuwa rahisi? Ilibidi kuwe na kitu fulani *hapa* chini kinachotembea, upendo halisi ambao hautashindwa. Akakilaza kichwa chake nyuma, akachomoa kisu kikubwa namna *hiyo*, wembe tu, kimenolewa kikawa kikali, akakivuta kichwa chake nyuma, akakitoa, akamwinulia Mungu, akashika sehemu ya juu ya nywele zake, akazishikilia nyuma namna *hiyo*, ndipo akainua mkono wake.

160 Yapata wakati huo Roho Mtakatifu akaushika mkono wake, “Shikilia tu mkono wako, Ibrahimu, ninajua unanipenda.”

161 Na yapata wakati huo kondoo dume akalia nyuma yake, hakuwa hapo sekunde moja hapo kabla. Kondoo dume alikuwa amenaswa pembe zake vichakani, amenaswa kichakani, “*Mee!*” Ibrahimu akaangalia kote, akaenda, akamchukua huyo kondoo dume, akamlaza juu ya madhabahu, akamfunga kwa kamba ambayo Isaka alikuwa amefungiwa, kisha akamchinja huyo kondoo dume.

162 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani: Huyo kondoo dume alitoka wapi? Ilikuwa angalau maili mia moja kutoka kwenye ustaarabu miongoni mwa simba, mbweha, kila namna, kila kitu kinachokula kondoo, mbwa mwitu. Na tena, alikuwa huko juu kabisa mlimani ambako hakuna chakula wala maji, wala hakuwepo wakati Ibrahimu alipokuwa akiokota mawe kote kutengeneza madhabahu, bali huyo hapo. Ee Mungu! Yehova-Yire, Yeye alikuwa amejitolea Mwenyewe mwana-kondoo kwa ajili ya hiyo sadaka. Naye ni Yehova-Yire yeye yule, usiku wa leo, jambo pekee ni kwamba, kwamba kwa huo Uzao sasa, wa Ibrahimu, Yeye tayari ametoa Mwana-Kondoo, Mwana-Kondoo tayari amechinjwa, Mwana-Kondoo anayetokwa na damu.

163 Sasa, hilo halikuwa ni ono ambalo Ibrahimu aliona, kwa sababu huyo kondoo dume alitokwa na damu, wala ono halitokwi na damu. Mnaona? Akamchinja huyo kondoo dume. Mungu alimnena akawa, naye Ibrahimu akamwondosha katika muda usiozidi dakika moja. Akawa, kisha akaondoshwa dakika iliyofuata, kwa sababu Mungu alikuwa na sababu kwa ajili

yake, kwa sababu alikuwa amemleta mtu fulani mahali hapo, akimjaribu. Biblia ilisema Ibrahimu alijaribiwa, nao Uzao wa Ibrahimu umejaribiwa. Sasa, Mungu alikuwa akimjaribu mtumishi Wake. Naye anaweza kuandaa ama kufanya chochote kwa njia yoyote atakayo, kwa sababu Yeye ni Yehova-Yire.

<sup>164</sup> Sasa, kama wewe ni mgonjwa, unateseka, vema, haidhuru una shida gani, kama Mungu amekufunulia kwamba utaninii . . . kwamba *umeponywa*, tayari, na Mwana-Kondoo Wake aliyetolewa, naye daktari anasema huwezi kupona, Yeye ni Yehova-Yire, Bwana anaweza kukupa macho, nimemwona akifanya hivyo, Bwana anaweza kukupa masikio, Bwana anaweza kukupa afya, Bwana anaweza kukupa nguvu, Yeye ni Yehova-Yire, dhabihu ya Bwana iliyotolewa. Na katika Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, haya yote yametimizwa kwa ajili yako, Uzao wa Ibrahimu, kama tu utaamini kama Ibrahimu alivyoamini. Je, unaamini?

Na tuinamishe vichwa vyetu basi.

<sup>165</sup> Je, wewe ni mgonjwa? Wewe ni mhitaji? Yehova-Yire yupo, Yeye Yule aliyeahidi mambo yote, akitoa ishara zote, akitimiza Neno Lake lote, yuko hapa katika ghala hili la silaha katika Middletown, Ohio, usiku wa leo. Kama unamhitaji, inua tu mkono wako. Sasa mweke niani mwako, ninapoomba.

<sup>166</sup> Baba wa Mbinguni, ninakuja katika Jina la Dhabihu Yako iliyotolewa ambayo niliikubali kama Mwokozi wangu. Naye akaubadilisha moyo wangu huu mwovu, katili, wa Kiairishi, umelazwa pale kitandani, ukiwa na dakika tatu tu za kuishi, kwa mtaalamu, moyo wangu ukipiga tu mara kumi na saba kwa dakika moja, lakini Yehova-Yire akaja jukwaani. Na hiyo imekuwa yapata miaka thelathini na mitano iliyopita, nilipokuwa na dakika tatu za kuishi, lakini Yehova-Yire akanipa uhai. Kwa nini nisiutumie, basi, kwa ajili Yake?

<sup>167</sup> Huenda kukawa na wengine hapa, usiku wa leo, Bwana, hapana shaka, labda si wagonjwa hivyo, bali nilikuahidi pale kwenye kitanda hicho cha hospitali ya kwamba kamwe sitakuonea aibu, kwamba ningelitetea Neno Lako, ningepiga mayowe kutoka paa za nyumba, pembeni mwa barabara, na kwa miaka thelathini na mmoja nimepiga makelele Bwana.

<sup>168</sup> Sasa mtumishi Wako anazeeka, ninakuomba Wewe, Bwana, ya kwamba utawabariki watu hawa usiku wa leo, na utawafanya waone kweli hii ya Injili. Kama vile mwandishi wa wimbo alivyosema:

Neema ndiyo iliyoufundisha moyo wangu  
kuogopa,  
Neema ndiyo iliniondolea hofu;  
Jinsi neema hiyo ilivyoonekana ya thamani  
Ile saa niliyoamini kwanza!  
Kupitia hatari nyingi, taabu na mitego,

Nimekwisha kuja;  
 Yehova-Yire ndiye aliyenileta salama umbali  
 huu,  
 Naye ataniongoza.

<sup>169</sup> Nipe imani usiku wa leo, ninapowaombea wagonjwa. Nisaidie, Bwana, na uwape watu imani ya kuamini. Sasa, hakuna kitu, Bwana, nimewaambia tena na tena, hakuna kitu ndani yangu, wala mtu mwingine yeyote anayeweza kufanya yale Wewe tayari umefanya, uponyaji wao umekamilika, Wewe uliwakomboa na ugonjwa wao ulipokufa kwa ajili yao. Ulijeruhiwa kwa makosa yao, kwa kupigwa Kwako waliponywa.

<sup>170</sup> Jalia wawe na imani usiku wa leo, Bwana, si kutumainia ustahilifu wa mhemko fulani waliokuwa nao, ama msisimko fulani, ama kitu fulani, lakini jalia waje na imani rahisi, dhahiri, na uamuzi dhahiri, “Usiku wa leo, ninamkubali Kristo kama Mponyaji wangu. Kutoka moyoni mwangu ninaamini Yeye huniponya.” Tujalie, Bwana, na yote yatakwisha. Tujalie, Baba. Ninaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>171</sup> (Tunapaswa kutoka saa ngapi? Kuna wakati wowote uliowekwa?) Kama ninyi nyote mtakuwa tu na kicho kabisa kwa dakika chache tu. Siamini tumekuwa na mstari wowote wa maombi ulioitishwa bado, siyo? Hatujaitisha mstari wa maombi tangu tumekuwa hapa. Nilikuwa tu, kutoka kwenye—kutoka—kutoka jukwaani? Si hivyo ndivyo ilivyokuwa? Hizo kadi za maombi zilikuwa zipi? A moja hadi mia moja?

<sup>172</sup> Je, ni afadhali muitwe kutoka madhabahuni hapa? Watu wasio na kadi za maombi waitwe hivyo, ama watu walio nazo? Haijalishi kwangu, njia yoyote itakayowaletea imani zaidi. Laiti mngalikuwa na imani na kuamini, msiwe na shaka, na mkae tu kwa kicho kabisa, mkae kimya.

<sup>173</sup> Sasa, huu ndio wakati, haidhuru nimehubiri kiasi gani, kama si kweli, si kweli. Mungu kamwe hatashuhudia uongo, mnajua hilo, bali kama ni kweli, Mungu anawajibika kushuhudia hilo.

<sup>174</sup> Sasa, ndugu zangu, dada zangu, je, tafadhalini, mnaweza kuendelea tu kuwa na kicho mwezavyo? Hebu tuite chache za kadi hizo. Tusipozipata usiku wa leo, zote, tutazipata kesho. Hebu tuchukue karibu dazani moja, ama kitu kama hicho, jukwaani, na halafu tuache Roho Mtakatifu, akipenda, aanzie kwenye kusanyiko.

<sup>175</sup> Ni wangapi huko nje wasio na kadi ya maombi nanyi ni wagonjwa? Inueni mikono yenu. Kila mahali. . . Loo, jamani! Ni wangapi walio na kadi za maombi basi? Inua mkono wako. Kuna wengine wasio na kadi za maombi, na kuna wachache tu walio na kadi za maombi. Labda baadhi yao jana usiku waliopata kadi za maombi, waliondoka.

<sup>176</sup> (Ulisambaza zipi, kutoka moja hadi hamsini, ama, kutoka moja—moja hadi mia moja, jana usiku?) Hebu tuanze, tuseme, sabini na tano. Hilo litakuwaje? Angalieni kama iko hapa. Kadi ya maombi namba sabini na tano, ni nani aliye na hiyo, inua mkono wako? La? Vema, tutaanzia mahali pengine. Loo, samahani. Vema, namba sabini na tano, vipi kuhusu wewe kuja papa hapa, mama? Namba sabini na sita, ni nani aliye na hiyo? Sabini na sita. Huyu mama? Njoo papa hapa. Sabini na saba, kadi ya maombi saba-saba. Huko nyuma. Sabini na nane. Njoo hapa, mama. Sabini na tisa, sabini na tisa. Je, niliiona? Je, iliinuliwa? Sabini na tisa. Themanini, ni nani aliye na kadi ya maombi themanini? Waweza kuinua mkono wako, ili tuweze kuona? Themanini.

<sup>177</sup> Sasa, mvulana anapokuja kugawa kadi za maombi, yeye husimama mbele zenu, anazichanganya pamoja. Hiyo si ni kweli? Kisha anachukua na kukupa kadi ya maombi, mtu yeyote anayetaka moja, mnaona, haijalishi. Kwa hiyo, hatujui tutawaita kuanzia wapi, wala hakuna ajuaye mpaka... Huyu mvulana hawezi kuwaambia, “Vema, tutaanza, usiku wa leo, kutoka namba moja. Nitakupa *wewe* namba moja, na *wewe* namba mbili, *wewe*...” Hawezi kufanya hivyo. Mnaona? Na inathibitisha hilo, maana yeye huzichanganya hapa mbele zenu. Uh-huh. Vema.

<sup>178</sup> Nilikuwa wapi, themanini? Themanini, kadi ya maombi themanini. Themanini na moja. Nilipata hiyo? Themanini na moja, themanini na mbili, themanini na tatu. Je, hiyo ndiyo...? La, alisimama kwa ajili ya mtoto mchanga. Themanini na tatu, waweza kuinua mkono wako? Nyuma upande wa nyuma. Themanini na nne. Vema. Themanini na tano. Sikuiona. Themanini na tano, themanini na sita, themanini na sita. Mwanamume huyo. Themanini na saba. Sikuiona. Themanini na saba.

<sup>179</sup> Angalia kadi ya jirani yako, labda yeye ni kiziwi. Loo, sawa. Themanini na saba, themanini na nane, themanini na nane. Ni gani, huyu mwanaume kipofu, namba yake ni ipi? Yeye ni—yeye ni...? Hiyo haingekuwa ndiyo namba yake, sivyo? Loo, naam, loo, naam, alikuwa, loo, ni—ni nyuma. Loo, hiyo ni sawa, ishikilie, nitaipata. Kaa tu nayo, nitapata...

<sup>180</sup> Themanini na tisa, tisini, tisini na moja, tisini na mbili, tisini na mbili. Siioni. Tisini na mbili. Labda baadhi yazo zilisambazwa jana usiku. Vema, mna za kutosha hapo.

<sup>181</sup> Kila mtu katika mstari huu wa maombi aliyesimama hapa, angalieni kwa muda kidogo tu sasa, ninawatakeni mwe na kicho kabisa sasa. Ni—ninii tu, hii ni Jumamosi usiku, mnaweza kulala mpaka wakati wa shule ya Jumapili asubuhi, sasa, si lazima mwende kazini. Kwa hiyo sasa, iweni na kicho kabisa kwa

dakika chache tu. Chukueni Ujumbe huu, msisahau Ujumbe huu sasa, uchukueni Ujumbe huu.

<sup>182</sup> Kila mtu katika mstari huu wa maombi asiyefahamiana nami, ambaye sijui chochote kukuhusu, inueni mikono yenu, nyote katika huu mstari wa maombi. Vema, bwana. Kila mmoja wenu katika mstari huo wa maombi, naomba umwahidi Mungu kwa uchaji ya kwamba kama Mungu atafunua mambo haya, kwamba utaahidi utamwamini, na kulishikilia kwa moyo wako wote? Unaamini? Na kama ninge kuja tu na kumwombea kila mmoja wenu, na kuwapitisha hapa . . .

<sup>183</sup> Endapo umefanya jambo lolote baya lisahihishe, sasa, kabla hujaingia mstarini. Unaona? Fanya hivyo. Sasa, kwa maana kumbukeni, hiyo dhambi na iwe juu yenu, si juu yangu.

<sup>184</sup> Sasa, ni wangapi katika kusanyiko usiku wa leo, wanaoamini ya kwamba Mungu ndiye Mponyaji, na anaweza kukuponya, na atakuponya, nawe una imani kwa ajili yake, usiku wa leo? Inueni mikono yenu kwamba ninyi ni wagonjwa. Sasa, mnaahidi, ninyi huko nje. . . ? Ni wangapi humu ndani wanaojua ya kwamba siwajui ninyi ambao ni wagonjwa, ama sijui lolote kuwahusu? Inua mkono wako.

<sup>185</sup> Sasa, kama Bwana Yesu atafanya yale hasa aliyosema alifanya wakati alipokuja hapa duniani, yale hasa aliyohidi yangetukia katika siku za mwisho, kama Yeye atatimiza hilo mara moja tu katika mstari huu wa maombi, ama wakati mmoja huko nje, mtaamini kwa uchaji, ninapomwinulia Mungu mikono yangu ya kwamba simjui yeyote wa hao watu hapo . . .

<sup>186</sup> Na kuna wachache hapa ninaowajua. Ninajaribu kumtambua mtu huyu aliyeketi hapa, nami ninaamini mtu huyu aliyeketi hapa amevaa suti nyepesi, nimemwona mahali fulani. Ndugu na Dada Kidd, ninawajua.

<sup>187</sup> Nami ninajua ya kwamba nina marafiki fulani hapa kutoka Jeffersonville, wamerudi hapa mahali fulani, mmoja wa mashemasi wa kanisa letu, Ndugu Fred Sothmann, yeye yupo hapa. Mwingine wa mashemasi, ama yeye ni mdhamini, mmoja wa mashemasi, mhubiri wa Kimethodisti, Ndugu Collins, alikuwa hapa hivi majuzi, yeye na mke wake wako hapa.

<sup>188</sup> Ndugu Welch Evans na familia yake kutoka huko chini Georgia. Hao watu huendesha gari, vema, safari ya kwenda na kurudi, ningesema ni yapata maili elfu moja mia nne, ama elfu moja mia tano kila Jumapili kunisikia nikihubiri huko Jeffersonville. Nena kuhusu marafiki! Kufa kwa ajili yako.

<sup>189</sup> Ndugu Tom Simpson, yuko hapa, nami nafikiri baadhi ya familia yake wako pamoja naye, yeye pia ni ndugu yangu aliyetutembelea. Ndugu Leo na Gene, wako hapa, wao ni wafanyakazi wenzangu hapa mkutanoni.

<sup>190</sup> Halafu nina rafiki hapa, Ndugu Rodney, na Ndugu Roger, na Ndugu Charlie, wanatoka hapa juu Ohio, mahali fulani, hapa juu karibu mpakani mwa Indiana, marafiki zangu binafsi. Ndugu wa Mwingano na Wamethodisti, ambao ndio kwanza waingie na kuokoka na kujazwa na Roho Mtakatifu, wa—wanapaswa kuwa hapa. Walikuwa hapa jana, nilikuwa na baadhi yao kwenye mahojiano ya faragha, nao wako hapa. Na nje ya hao, hakuna mtu ninayeweza kumwazia.

<sup>191</sup> Ndugu Dauch, aliyeketi hapa, ni—ninamjua. Ni jina la Kijerumani, Ndugu Dauch, si—siwezi kulitamka, ni *Dauchs*, ama Dauch, ama kitu kama hicho. Ndugu mzuri sana kutoka papa hapa Ohio, amekuwa baraka kubwa kwangu.

<sup>192</sup> Naye mtu huyu aliyeketi papa hapa nyuma, amevaa tai nyekundu, aliyeketi papa hapa, *wewe*, moja kwa moja chini, hivi sikujui? La, mtu aliyepapa hapa nyuma yako, hapo, hivi sikujui? Ni—ni—nilifikiri ninakujua. Siwezi kukumbuka jina lake, bali ni—ninamjua.

<sup>193</sup> Na hivi majuzi asubuhi, Roho Mtakatifu alikuwa akiniongoza barabarani, nikaingia chumbani kula kiamshakinywa, *Kitu fulani* kikasema, “Usiende. Shuka uende mtaani.”

<sup>194</sup> Nikaanza kutembea mtaani, nami nikashangaa, “Kwa nini? Kwa nini?” Nikaendelea kutembea barabarani, ndipo nikawaona mama wawili wamesimama pembeni, nikaendelea kutembea, nikawaza, “Baba, ungetaka nifanye nini?”

“Endelea tu kutembea.”

Ndipo niliposhuka kwenda pale, wanawake hawa wakageuka, na kusema, “Bwana, waweza kuniambia lilipo duka la vyakula?”

Nikasema, “La, mimi ni mgeni hapa.”

Nao wakaangalia kote, kasema, “Hivi wewe siye Ndugu Branham?”

Nikawaza, “Hili hapa.”

<sup>195</sup> Maskini mwanamke mmoja alikuwa akiomba kwa bidii sana anione faraghani. Akatoka akaenda pembeni kungojea, Mungu alimtuma huko nje, kisha Mungu akanituma nitoke chumbani mwangu nishuke chini. Ameketi papa hapa sasa, papo *hapo*. Akaniambia kuhusu jambo fulani alilotaka kunizungumzia faraghani. Mnaona? Wewe, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kufuata uongozi wa Roho. Yeye hufanya kazi kwenye ncha zote mbili za mstari, analifanya sawa kabisa. Mnaona? Kweli kabisa.

<sup>196</sup> Na kama ningewaambia watu kutoka Jeffersonville, mimi—mimi, vema, nisingewaita kama ningeona, isipokuwa iwe ni kitu ambacho wangeninii... Ingenibidi kuwaambia ama chochote kile, lakini kwa kawaida, ni hao watu wengine.

Ninyi nyote ombeni sasa, na mwamini kwa moyo wenu wote.

197 Sasa, mwanamke mmoja alifanya nini . . ? Yesu alimwambia shida aliyokuwa nayo, naye akaingia na kuwaambia, ndipo mji mzima ukamwamini Bwana, kizazi kizima, kabila zima la watu, wakaamini ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi.

198 Sasa, mimi siye Masihi, mnajua hilo. Loo, jamani, mimi ni mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema, mimi ni mwanadamu, bali Masihi hufanya kazi katika wanadamu. Sasa, kama nilivyokuwa nikijaribu, kuwaambia, hakuna Miungu watatu, mtu yeyote aaminiye hilo ni mpagani. Kuna Mungu mmoja tu, Yeye anaishi katika ofisi tatu. Ubaba . . . Loo, watu wameingia wazimu wakijaribu kusoma hilo. Mbona, ni rahisi sana, Mungu, Baba, kipindi cha wakati wa Baba, Uwana, Roho Mtakatifu, Mungu yeye yule.

199 Si Miungu watatu, Mmoja aitwaye Baba, na Mmoja anayeitwa Mwana, Mmoja anayeitwa Roho Mtakatifu. Ha! Ukiamini hilo, ndugu, afadhali uende kwenye kanisa Katoliki, hapo ndipo mahali pako, hasa kabisa, huko ndiko lilikotoka. Hakuna fundisho kama hilo katika Biblia, hakuna kitu kama hicho, *utatu* hata haujatajwa katika Biblia, hata wakati mmoja.

200 Sasa, mimi si . . . usininii . . . na ninasema . . . Na baadhi ya watu wanasema, “Yeye ni wa *Yesu Pekee*,” umekosea hapo, nisingekuwa na roho ya namna hiyo juu yangu, pale, jambo hilo la sharti, lisilo la kiungu ambalo . . . la, bwana. Mimi si wa *Umoja*, hata kidogo, wala mimi si wa *Utatu*, mimi ni Mkristo, ninamwamini Mungu. Ninaamini katika Mungu aliyedhihirishwa katika ofisi tatu. Sasa ofisi Yake iko moyoni mwangu, moyoni mwako, si Mungu mwingine mahali pengine, Mungu mwingine mahali pengine, Mungu mwingine mahali pengine, huo ni upagani kadiri upagani uwezavyo kuwa. Hakuna hata wakati mmoja hilo lilipowaziwa mpaka kwenye Baraza la Nikea, litafute katika Biblia, ama ulitafute katika historia, mpaka wakati huo, halipo.

Gene, wewe ndiwe utakayeniletea mimi? Vema, Ndugu.

201 Sasa, kama mtu yeyote humu ndani anashuku kwamba hili si la Mungu, mna mfumo bora zaidi wa kuwasaidia watu hawa, kwa uchaji wote wa kiungu, na heshima za kindugu, nitaketi hapa chini pamoja na Ndugu Sullivan, kuja jukwaani, unaweza kufanya jambo lolote tofauti kulihusu. Ama kama unataka kuja kufanya jambo lile lile, kama unafikiri kwamba mimi ni wa ibilisi, nawe ni wa Mungu, basi hakika unaweza kulishinda hili, unaweza kumshinda ibilisi kama wewe ni wa Mungu, basi njoo, uchukue mahali hapo. Si kwamba mimi Ndiye, bali Yeye yupo hapa. Sasa, haidhuru nini, angenipaka mafuta kiasi gani, hana budi kukupaka mafuta vivyo hivyo.

202 Sasa huyu hapa amesimama mwanamke ambaye sijawahi kumwona maishani mwangu, yeye ni mgeni kabisa kwangu

mimi, sijawahi kumwona, yeye ni mwanamke tu aliyesimama hapo. Nami nadhani hii ndiyo mara ya kwanza tumewahi kukutana, nijuavyo mimi. Hiyo ni kweli? [Huyo dada anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Hiyo ni kweli. Sasa, kama hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana, nami nginginua mikono yangu kwa hilo. Kama niliwahi kukutana nawe, mimi... ilikuwa mahali fulani ambapo sikujua wewe ni nani, tulipitana mtaani, ama uliketi mkutanoni, ama kitu kama hicho, ni—nisingekujua kwa njia nyingine yoyote. Lakini kukujua tu, sikujui, wala hunijui, bali kuna Mtu fulani hapa anayetujua sote wawili, hiyo ni kweli, Mtu fulani anatumujua sote wawili. Sasa tutajisahau na kumwacha Yeye anene kupitia kwangu, na...

<sup>203</sup> Sasa, kama nikija hapa, na kusema, “Mama, wewe ni mgonjwa. Haleluya! Mungu asifiwe! Nenda ukaponywe, umeponywa. Endelea.” Sasa, hilo lingekuwa sawa, kama unataka kuliadini, unaponywa tu kwa imani. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo sasa, ungeweza kuwa na haki ya kushuku hilo, bali juu ya Maandiko, yale niliyowaambia ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho, na Mungu yeye yule aliyeishi katika mwili wa mwanadamu, wakila na kunywa kule, ambao miaka mia kadhaa baada ya hilo kudhihirishwa katika mwili, Mungu yeye yule, maana Yeye alikuja kwa ajili ya Ukombozi kumtafuta mtoto Wake aliyepotea...

<sup>204</sup> Mungu aliposhuka katika bustani ya Edeni, kwa nini hakumtuma Malaika kumtafuta Adamu? Kwa nini hakumtuma Mwana fulani kumtafuta Adamu? Huyo alikuwa ni mtoto Wake aliyepotea, Yeye alikuja Mwenyewe. Hiyo ndiyo sababu Yesu alikuwa ni Mungu aliyefanyika mwili, alikuja katika mwili wa mwanadamu kukukomboa. Nilikuwa nikitaka kuzungumza juu ya hilo usiku wa leo, kama sikuwa nimemaliza huo jana usiku, *Mkombozi Wa Jamaa*, kuonyesha ya kwamba alikuwa hivyo, ilibidi awe mwanadamu. Kwa hiyo, kupitia Damu hiyo, bila kujuana kimwili, hiyo Damu isiyoghoshiwa, iliyumbwa na Mungu, ninasimama hapa usiku wa leo, nikiwa na changamoto hii—hii juu ya Biblia yangu, nikisimama mbele ya mwanamke mmoja, kusema ya kwamba Mungu hutimiza Neno Lake, hapo ndipo tunaposimama.

<sup>205</sup> Kama Mungu atanifunulia jambo fulani ambalo unajua kwamba mimi... Kama—kama kuna jambo lolote kukuhusu, silijui. Lakini kama Yeye atanifunulia, basi utajua, na kama yule mwanamke kwenye kisima cha Samaria, uende ukawaambia watu wako kwamba, “Njoni mwone Mtu,” sio Ndugu Branham, sasa, bali, “Bwana Yesu aliye Kanisani Mwake, akijidhihirisha Mwenyewe, kwa sababu aliniambia mambo yaliyo maishani mwangu.” Je, ungekuwa tayari kufanya hivyo?

Je, kanisa lingekuwa tayari kufanya hivyo?

<sup>206</sup> Kwa kweli husimami hapa kwa nafsi yako, ni kwa ajili

ya mtu mwingine. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaona? Yeye anajua kilicho moyoni mwako. Ikiwa Mungu, basi, atanielezea, ama kuniambia jambo fulani kuhusu hili, ama mtu fulani, utaniamini? Mtu huyo, si hapa, wako katika hali ya kufa kwa kansa, nawe umesimama kwa ajili yao. Hiyo ni kweli? Unajua lesa hiyo uliyo nayo mkononi mwako, hapo? Wapelekee hiyo. Wala usiwe na shaka. Hutaalitilia shaka? [Dada anasema, “La.”—Mh.] Basi unaweza kupata kile unachoomba. Mungu akubariki. Mungu akubariki.

Sasa, kanisa linaamini? Kama unaweza kuamini! Linawatikisa wengine, wengine haliwatikisi. Hakuna kitu. . .

<sup>207</sup> U hali gani? Ikiwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, atanifunulia kilichokuleta hapa, ama unayemsimamia, ama *kitu kingine*, utajua kama ni kweli ama si kweli, siyo? Utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, nami nimekwambia kweli juu ya Neno la Mungu. Uko tayari kwa mshtuko? Wewe ni mahututi, umetiwa uvuli wa mauti, weusi juu yako, kansa. Ni kansa ya mapafu ambayo imepitia kwenye mfumo wako. Hiyo ni kweli. Njoo hapa. Ikiwa Roho wa Mungu aliyeifanya Biblia. . . Agizo la mwisho ambalo Mwokozi wetu alilipa Kanisa, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sasa, unajua *Kitu fulani* kimenitia mafuta, hiyo ni kweli? Vema basi, kama nikikuwekea mikono na kumhukumu ibilisi huyo, utaamini hilo, kwamba linatoka kwa Mungu, Mungu yeye yule anayejua kukuhusu? Basi unaweza kuishi.

<sup>208</sup> Mwenyezi Mungu, Mwumba wa mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa Milele, na Mpaji wa kila karama njema, huku mikono imewekwa juu ya mwanamke huyu, kama agizo la mwisho alilopewa Bwana wetu, ama, na Bwana wetu, ambalo Kanisa Lake linapaswa kufanya, ninalaani mauti hii inayoning’inia juu ya mwanamke huyu, na kumwacha aishi, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Sasa, niandikie ushuhuda wako; amini kwa moyo wako wote.

U hali gani? Unaamini Mungu huponya ugonjwa wa rektamu, pia? Vema, umekwisha basi. Uligusa nini basi? Ulingusa Yeye.

<sup>209</sup> Sikujui, Mungu anakujua. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Ninajaribu tu kuninii. . . Mnaona, Malaika wa Bwana (Uliwahi kusoma kitabu changu?), alipokutana nami usiku ule, kasema, “Ukiwafanya watu wakuamini.” Waniamini mimi, kitu gani? Kwamba nimesema kweli. Nilisimulia hadithi ya Biblia, kwa hiyo hiyo haina budi kuwa ni kweli. Kama Bwana atanifunulia jambo fulani kukuhusu wewe, utaamini ni. . .? Itakubidi kujua kama hiyo ni kweli ama si kweli. Unaugua ugonjwa wa kibofu nyongo. Hiyo ni kweli.

<sup>210</sup> Hili hapa linakuja. Ninii tu, mimi tu, inaonekana kana kwamba ninatarajia hilo, “Alibahatisha hilo.” Sikubahatisha hilo, acha kuwazia hilo. Mimi. . . Nakufanya ujionee aibu sasa!

<sup>211</sup> Sijui alichokwambia. Hebu kidogo. Naam, hiki hapa, kiko chini ya mbavu hapa, ni kibofu nyongo, hiyo ni kweli, husababisha maradhi na maumivu ya tumbo, na kila kitu. Hiyo ni kweli. Pia una mishipa iliyovimba, unaugua ugonjwa wa wasiwasi, una matatizo, ndivyo asemavyo daktari. Jina lako ni Bibi Osborne. Nenda nyumbani ukawe mzima, Yesu Kristo anakuponya.

<sup>212</sup> Aibu kwenu! Mwaminini Mungu. Msiwe na shaka. Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.

<sup>213</sup> Mama huyo aliyeketi hapo na nywele zake zimefagiliwa juu *hivi*, akiniangalia moja kwa moja, kuna kitu fulani, wakati Hiyo ilipomgusa mwanamke huyu, ilimgusa mwanamke huyo, pia, nami nikaangalia kote, nikaona hiyo Nuru juu yake, sijui. Tatizo alilo nalo mwanamke yule, ambaye ndiyo kwanza aondoke jukwaani, ndilo tatizo la mwanamke huyo, pia. Unaugua, sivyo, dada, mgonjwa? Naam, ninaliona sasa. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Una ugonjwa wa kibofu nyongo. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema, umeponywa, Yesu Kristo anakuponya.

Unaamini?

<sup>214</sup> Kama unataka kuniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake: hiyo ilimgusa rafiki yako aliyeketi hapo karibu sana na wewe, pia ilimponya ugonjwa wa matiti aliokuwa nao. Huh! Unaamini hilo mama? Unalikubali? Inua mkono wako kama unalikubali. Vema. Nenda nyumbani ukiamini, unaweza kuponywa. Ninawaomba tu kuamini, hivyo tu.

Yeye yuko katika hili kusanyiko.

<sup>215</sup> Mnawona maskini mama huyu aliyeketi hapa akiomba kwa moyo wake wote? Hajiombei mwenyewe, anaombea da—dada aliye na kansa. Naam. Kwa namna fulani hisia ya ajabu sivyo? Vema. Sasa nenda, amini. Hilo ni sawa.

<sup>216</sup> *Hmm!* Ajabu, mwanamke mwingine alitokea karibu Naye, Yeye yuko moja kwa moja nyuma yake pale, akiombea jambo lile lile. Wewe amini pia, Dada, unaweza kupata wako.

<sup>217</sup> Loo, niambieni waligusa nini? Jinsi gani? Wako futi ishirini kutoka kwangu, ama thelathini, wangewezaje kunigusa mimi? Hawakunigusa kamwe, bali walimgusa Kuhani Mkuu, Yesu Kristo, awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.

<sup>218</sup> Sikujui wewe, hatufahamiani. Kama Bwana Yesu atanifunulia jambo fulani. . . Unatambua uko Mbele Zake, kosa moja, ungeweza kuanguka ufe kwake, unajua hilo. Hiyo ni kweli. Utaamini kwa moyo wako wote? Shida yako iko mgongoni mwako. Hiyo ni kweli. Figo lililoenda kombo. Hiyo

ni kweli. Unaamini utaponywa? Bibi Combs, unaweza kwenda nyumbani, na uwe mzima. Mwombee mwanamke huyo, hapo, uh-huh. Ni imani yako.

<sup>219</sup> Sikujui. Loo, vipi—vipi—vipi kama...? Loo, sawa. Unafikiri mama yako atatoka kwenye kiharusi hicho, na awe mzima? Vema. Nenda, amini, unaweza kuponywa. Mungu akubariki.

<sup>220</sup> Mungu anaweza kuponya kansa, na kukupa afya? [Dada huyo anasema, “Ninaamini.”—Mh.] Vema. Nenda, amini kwa moyo wako wote, na upate afya. Kama unaweza kuamini!

Njoo, mama. Kuna yapata asilimia themanini ya kusanyiko hili wanaougua kitu kile kile, mama. Hebu nikuonyeshe.

Ninyi nyote huko nje mnaosumbuliwa na wasiwasi, inueni mikono yenu, kila mtu.

<sup>221</sup> Unaona? Hiyo ndiyo shida yako. Inatokea yapata wakati huu wa maisha kwa vyovyote vile, lakini umekuwa na wasiwasi kwa muda mrefu. Unaamini umeushinda sasa? Nenda ukimshukuru Bwana. Sema, “Asante, Bwana Yesu.”

Je, Mungu anaweza kuponya mgongo wako, na kukupa afya? [Ndugu huyo anasema, “Naam.”—Mh.] Vema. Nenda tu uamini basi, kwa moyo wako wote.

Ninaona shida yako, lakini hivyo sivyo ilivyo, una wasiwasi sana hata hujui jinsi ya kujishikilia pamoja. Nenda, amini, itakuwa sawa.

<sup>222</sup> Huyu...mama yuyu huyu hapa alikuwa na ugonjwa wa wasiwasi, ana matatizo mengine, matatizo, lakini kwa kweli anataka niombee mishipa. Hiyo ni kweli? Amini, na uende ukaponywe. Amini tu kwa moyo wako wote.

<sup>223</sup> Sikujui, sivyo? Unaamini Mungu ataponya ugonjwa huo wa kike ulio nao, akupe afya? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Basi nenda, amini, uwe na imani.

Mnaamini huko nje, kila mmoja wenu? Mna imani?

<sup>224</sup> Huyu mama aliyeketi papo hapo ana shida ya kike, pia, anayoombea. Hiyo ni kweli. Mama, kwa namna fulani, uliye na kitu fulani pajani mwako. Hiyo ni kweli. Wewe, wewe! Uligeuka ukamwangalia mwanamke mwingine. Amini! La, papa hapa, wewe uliyeweka mkono wako nyuma namna *hiyo*, amini kwa moyo wako wote. Nenda nyumbani, naam, bwana, ukaponywe. Yesu Kristo huponya.

<sup>225</sup> Unawazia nini, huko nje ukimwombea mke wako ambaye amerudi nyuma? Unafikiri atarudi nyumbani, na kuwa... Simama kwa miguu yako. Vema. Ninamrudisha kwako, katika Jina la Yesu Kristo.

Nenda, amini, Dada, uponywe. Yesu Kristo akuponye, na kukupa afya.

<sup>226</sup> Sasa, hivyo karibu ndivyo inavyombidi kutoka kitandani asubuhi, pia. Uh-huh. Ni yabisi kavu, bali Mungu anaweza kuponya yabisi kavu, sivyo? Vema, kama wewe. . . Vema, nenda tu ukamwamini, basi. Nenda tu, useme, “Asante, Bwana.” Mwamini Yeye.

<sup>227</sup> Vipi kama hata sikukwambia jambo moja, nilisema tu. . . niliweka mikono yangu juu yako, unaamini ungepona? Njoo basi. Mungu akubariki. Nenda, ukaupokee, Dada, katika Jina la Yesu.

<sup>228</sup> Sasa, hii hapa inakuja tena, ugonjwa mwingine wa mishipa. Hiyo ni kweli. Ni wangapi kwenye kusanyiko huko nje, kwa moyo wako wote, kwa yote yaliyo ndani yako, nawe unaamini kwa nguvu zote ulizo nazo kwamba Mungu ni Mponyaji wa wasiwasi? Inueni mikono yenu namna *hiyo*. Kama anaweza kumponya mwanamke huyu hapa. . . Sasa, kupitia hiyo. . .

<sup>229</sup> Njoo hapa kwa dakika moja. Um-hum, una matatizo mengine madogo pia, sivyo? Ya kike. Unaona jinsi ningeweza kujua jambo hilo? Kukuonyesha jambo fulani, angalia hapa, anapoweka mkono wako juu ya wangu, angalia hapa, unaona mkono wangu? Unaona jinsi unavyoonekana wa kawaida, kama mkono wa mtu yeyote? Sasa, weka mkono huu hapa. Sasa, uangalie. Unaona jinsi unavyovimba, na vitu hivyo vidogo vyeupe vinapita juu yake? Sasa, angalia, weka mkono huu mwingine hapa na uweke juu yake. Haifanyi hivyo kwa huo, sivyo? Haifanyi hivyo kwenye huo. Vema, kwa nini ufanye tu juu ya huu, basi? Hiyo ilikuwa ndiyo karama ya kwanza niliyopewa, unaona, ni mawasiliano yako, mkono wako wa kuume kwa mkono wangu wa kushoto, unaahidi imani yako, kwamba unaamini ninayokwambia. Ninachukua mkono wako wa kushoto, na kumwinulia Mungu wangu, mkono wangu wa kushoto uko kwenye moyo wangu. Unaona?

<sup>230</sup> Sasa, unaona jambo fulani likitukia, inaonyesha kimwili shida iliyopo hapo. Hiyo si ni kweli? Sasa, kama wewe, hiyo ni kweli, unawaambia watu. Hiyo ni. . . ?

Angalia wakati anapoangalia hapa. Angalia mkono wangu wewe mwenyewe.

<sup>231</sup> Sasa ondoa mkono wako hapo. Sasa chukua mkono huu mwingine, uweke juu yake. Haufanyi hivyo hapo. Wewe ni mwanadamu tu katika mkono *huu* kadiri ulivyo katika mkono *huu*. Unaona? Sasa basi, unaona kuna kitu kinachoonyesha kimwili, ambacho ni upako, hiyo ni kwa ahadi.

<sup>232</sup> Sasa wewe njoo hapa, sasa wewe angalia mkono wangu. Unaamini sasa, kwa moyo wako wote? Nitaweka mkono wangu papa hapa upate kuuona. Sio wewe. . . Unaona, si mahali ninaposhikilia mkono wangu, popote ulipo, vivyo hivyo tu. Sasa, kama huo ukiondoka, kama ukirudi kama mkono huu mwingine, vema basi utakuwa. . . utajua jambo fulani limetukia, sivyo?

<sup>233</sup> Sasa, sijui kama mnaweza kuliona au la, anapoweka mikono yake juu ya wangu, unavimba, na vitu vidogo vyeupe vikifanya, “*Rrrr, rrrr, rrrr.*” Hatambui, anajua ana shida ya kike, bali hajui ni nini. Mnaona? Ni uvimbe. Unaona? Sasa, hiyo hapo, inasonga. Amekuwa na matatizo kule. Sasa, sasa angalieni, nitaondoa mkono wangu kwake, angalieni mkono wangu sasa. Sasa, hebu achukue mkono huu mwingine *hapa* na kuuwekelea mkono huo. Hakuna hata chembe moja ya tofauti. Mnaona? *Huu* hauonyeshi, *huu* unaonyesha. Hiyo ni kweli, mama? Uko hapa kuliangalia. [Dada huyo anasema, “Ni kweli, ndiyo, bwana.”—Mh.] Unaona? Vitu vidogo vyeupe vikipitia mkononi mwangu, vikifanya, “*Rrrr, rrrr, rrrr.*”

<sup>234</sup> Ni kitu gani hicho? Huo ni uhai ndani yake ambao si wake. Sasa, daktari anauita *uvimbe, kansa*, kadhalika namna hiyo, bali Yesu aliuita *ibilisi*. Ati nini? Ni uhai. Huo ni nini? Ni uhai, kuzudishwa kwa seli. Uvimbe ni nini? Kuzidishwa kwa seli. Kansa ni nini? Kuzidishwa kwa seli. Mtoto wa jicho ni nini? Kuzidishwa kwa seli. Mnaona, huo ni uhai humo ndani. Ni upako hapa sasa wa Uzima wa Milele, na kuna Uzima hapa ambao ni Uzima wa Milele, na kuna uhai mle ambao ni mauti. Mnaona? Kwa hiyo hiyo ndiyo tofauti.

<sup>235</sup> Huyu mwanamke ni mwaminio. Mnaona? Ana wasiwasi, amekuwa hivyo kwa muda mrefu, hasa sana tangu kukoma hedhi, ana uastigmati machoni mwake, ana vipindi vya kizunguzungu. Loo, jamani, hilo ni rahisi. Mnaona? Lakini jambo ni kwamba, ni kuangalia sasa, na kuona. Sasa, siwezi kuufanya uondoke, ama, siwezi kuufanya ukae mbali.

<sup>236</sup> Sasa, ninataka tu kuushikilia mkono wangu mpate kuona yale niliyozungumzia muda mfupi uliopita ni kweli. Mnaweza kunisikia? Nitaushikilia mkono wangu hapa, na kumwacha tu huyu mwanamke aombe aone kama utaondoka. Omba tu, useme, “Bwana, nisaide.” Sasa, yeye anaomba. Mnaona? Sasa, hebu aangalie mwenyewe, sijauangalia mkono wangu. Bado upo. Mnaona? Sasa, nitaomba:

<sup>237</sup> Baba Mungu, sikia maombi yangu, ninamwomba mwanamke huyu ya kwamba utamsaidia, kulingana na imani yake. Amina.

<sup>238</sup> Haukuondoka, sivyo? Bado upo. Sasa, sitasogea, wewe angalia tu mkono wangu. Sasa, niwaonyeshe tu kile Yeye alichosema, nitahakikisha kwamba ni Yeye sasa. Sasa, Yeye aliniambia nini? Aliniahidi jambo hili. Siwezi kuufanya umwondokee, lakini kama akiuona ukiondoka yeye ataninii... Sasa, ninawatakeni mwangalie mkono wangu. Wewe, angalia mkono wangu.

<sup>239</sup> Mwenyezi Mungu, si kufanya maonyesho hapa, lakini hii labda itakuwa ndiyo mara yangu ya mwisho katika mji huu. Ninakuomba Wewe, Bwana, ujitambulishe Mwenyewe, ya

kwamba nimewaambia watu hawa ukweli, wanauangalia mkono wangu, huyu mwanamke anauangalia, pia. Lakini Maneno Yako ni ya kweli sana. Wakati mwingine wakati uchovu mdogo, fadhaa huzuia. . . Lakini ahadi Yako ingali inabaki kuwa kweli, “Katika Jina Langu watatoa pepo.” Sasa, Wewe uliahidi hilo, ulinithibitishia kwa Malaika usiku ule huko Green’s Mill, nikisimama kwenye kile kibanda.

<sup>240</sup> Shetani, huwezi kumshikilia tena, toka ndani yake, katika Jina la Yesu Kristo.

<sup>241</sup> Sasa hebu huyu mama awe ndiye hakimu, umeondoka. Umeondoka, mama? [Dada huyo anasema, “Kabisa.”—Mh.] Sijausogeza mkono wangu, sasa angalia, umeondoka. Weka mkono wako mwingine juu yake. Haupo, sivyoy? Umeponywa.

<sup>242</sup> Mnaona ninalomaanisha? Mnaamini? Sasa, ni waaminio wangapi waliopo hapa? Inua mkono wako. Hivi Biblia haijatangaza jambo hilo? Hivi Mungu hajafanya kazi na Uzao wa Ibrahimu sawa na alivyofanya na Ibrahimu? Si Malaika yule yule aliyekutana na Ibrahimu kwenye—kwenye, kwenye wakati tu wa Sodoma, kabla haujaangamizwa, si hizo ni kazi zile zile hapa, anazofanya usiku wa leo? Ni zile zile? Ndivyo? Mnaamini hilo? Je, ninyi ni Uzao wa Ibrahimu? Mungu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

<sup>243</sup> Ni wangapi huko nje walio wagonjwa? Inueni mikono yenu. Ni wangapi walioketi karibu nao ambao ni waaminio? Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi. Hivyo tu, weka tu mikono yako, hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya. Hiyo ni. . .

<sup>244</sup> Sema tu, unasema, “Vema, Ndugu Branham, ni—ninataka kubatizwa.” Ngingekubatiza tu, hivyo tu, ndipo unabatizwa. Hiyo ni kweli? Basi wewe ni Mkristo. Vema basi, kama ukisema, “Vema, Ndugu Branham, tubuni, mkabatizwe.” Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe, aminiye *na* kubatizwa ataokoka.” Hiyo ni kweli? Vema basi, kama ukiamini, na kubatizwa, Biblia ilisema umeokoka. Hiyo ni kweli?

Utaratibu wa ubatizo ni upi? Kuwazika tu chini ya maji, kuwatoa tena, wamebatizwa.

Ni utaratibu gani, basi, kwa wagonjwa? “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

“Ati kama Ndugu Branham akiweka mikono yake?”

Kamwe hakusema, “Ndugu Branham,” Yeye alisema, “yeyote.”

<sup>245</sup> Kwa hiyo ishara hizi zitafuatana na *hao* waaminio. Wewe ni mwaminio, kama nilivyo mimi, una haki zile zile za kuwekea mtu yeyote mkono wako kama nilivyo nazo. Kila

mmoja wa wahudumu wenu, wachungaji hawa, mtu mwingine yeyote, wana haki ya kufanya hivyo. Unaamini hilo? Basi ninawatakeni mwekeane mikono, uinamishe kichwa chako, usijiombee sasa, wewe mwombee mtu mwingine uliyemwekea mikono, maana wanakuombea. Wewe amini hilo kwa moyo wako wote. Ninawakabidhi kwa Yesu Kristo, ninapoombea vitambaa hivi hapa na lesa.

<sup>246</sup> Baba wa Mbinguni, lesa hizi ambazo nimeletewa, watu wanaamini kama tu walivyoamini katika siku za Paulo. Walimwona Paulo akiwa na hayo maono, nao walijua ya kwamba a—alitumwa na Mungu; watu hawa wanaamini jambo lilo hilo. Sasa Bwana, Wewe ni Mungu yeye yule kwetu, kwa sababu Ibrahimu alikuwa baba wa mataifa mengi. Nao walileta kutoka kwenye mwili wa Paulo, lesa, nguo, nazo zikapelekewa wagonjwa na wanaoteseka, nao pepo wakawatoka hao watu, pepo wachafu, magonjwa yaliponywa. Sasa, ninamkemea kila ibilisi... 

61-0318 Agano la Ibrahimu Likithibitishwa  
National Guard Armory  
Middletown, Ohio Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)